

# MWONGOZO WA LESENI

# YA DEREVA WA IOWA



ANGALIA MWONGOZO WA LESENI YA DEREVA WA IOWA MTANDAONI KWENYE  
[IOWADOT.GOV/DRIVERSMANUAL](http://IOWADOT.GOV/DRIVERSMANUAL)



*Kim Reynolds*

Kim Reynolds, Gavana wa Iowa

## UJUMBE MUHIMU KWA MADEREVA

Kuushika usukani kwa mara ya kwanza kunaweza kuwa kwa kuogofya, lakini hali ya kuisimua. Kuwa na uhuru wa kujiendesha kunafungua dunia mpya yenye fursa, lakini kujitayarisha na kujua sheria za barabarani kabla hujawasha gari kutaimarisha usalama kwetu sote tunaotumia barabara.

Kusoma, kuelewa na kutekeleza vipengee vilivyo katika mwongozo huu wa dereva kutakutayarisha katika safari yako ya kuwa dereva salama. Maelezo yaliyo katika mwongozo yatafafanua zaidi, lakini sheria za usalama za msingi zifuatazo zitakuwezesha kuwa tayari kuanza.

- Jifunge mkanda, haijalishi mahali unapokaa ndani ya gari.
- Tii kikomo rasmi cha kasi.
- Makinikia zaidi jukumu lako la kuendesha gari.
- Endesha gari kwa makini.

Asante kwa kutenga muda kujifunza vipengee vya utendaji katika mwongozo huu na kuvichanganya na mazoezi kwenye usukani. Hali hizo mbili za mafunzo na ahadi yako ya kuwa dereva salama vinathaminiwa na wale wote wanaotumia barabara za Iowa.

## KUTEMBELEA ENEO LA HUDUMA ZA LESENI YA DEREVA NA KITAMBULISHO

Kuna maeneo ya huduma katika jimbo zima kwenye Vituo vya Huduma vya DOT na Ofisi za Hazina ya Kaunti za Iowa. Unaweza kutembelea eneo lolote; si lazima liwe lile lililo karibu na mahali unapoishi. Vilevile, baadhi ya huduma, kama vile kujisajili tena kwa leseni, zinapatikana mtandaoni ikiwa una umri wa miaka 18 au zaidi na unakidhi matakwa mengine.



### RATIBU MIADI KWENYE ENEO LA DOT:

[www.iowadot.gov/service-selector](http://www.iowadot.gov/service-selector)



### KWENYE OFISI YA HAZINA YA KAUNTI:

Tumia tovuti iliyo hapa chini kuwasiliana na eneo unalopanga kutembelea ili kuona jinsi wanavyoendesha shughuli.

[www.iowadot.gov/mvd/iowa-dot-locations](http://www.iowadot.gov/mvd/iowa-dot-locations)



### MTANDAONI:

Angalia ili uone ikiwa unastahiki huduma za mtandaoni.

[www.mymvd.iowadot.gov](http://www.mymvd.iowadot.gov)

Hapa ndipo mahali TU unapoweza kujisajili tena kwa leseni yako mtandaoni. Kuna tovuti kadhaa huko nje zinazouza taarifa tunazotoa bila malipo. Hukufanya ufikirie kwamba unapata leseni mpya ya dereva, kumbe sivyo.



### JE, UNAHITAJI MWONGOZO HUU KATIKA LUGHA TOFAUTI?

Mwongozo huu unapatikana katika lugha za ziada kwenye:

[iowadot.gov/mvd/driverslicense/driverslicense/dlmanual](http://iowadot.gov/mvd/driverslicense/driverslicense/dlmanual)

# JEDWALI LA YALIYOMO

## **SURA YA 1: LESENI YAKO YA DEREVA.....4**

1.1 Je, ni nani anayehitaji leseni ya dereva ya lowa?.....	4
1.2 Kubeba leseni na bima yako.....	5
1.3 Uchunguzi na vipimo vya afya vinavyohitajika.....	5

## **SURA YA 2: ALAMA NA SHERIA ZA BARABARANI.....6**

2.1 Alama za barabarani.....	6
2.2 Alama za udhibiti.....	8
2.3 Alama za kuonya.....	9
2.4 Alama ya gari kuendeshwa polepole.....	10
2.5 Alama za mwongozo.....	10
2.6 Alama za huduma.....	10
2.7 Alama za njia.....	10
2.8 Taa za trafiki.....	10
2.9 Vivuko vya reli.....	11
2.10 Maeneo ya kazi.....	13
2.11 Alama za njia ya miguu na vidhibiti vingine vya kijia.....	14
2.12 Mistari ya kuachia njia.....	14
2.13 Vivukomilia, mistari ya kusimama na alama za mishale ya kuelekeza.....	14
2.14 Vijia vya kupindukia.....	14
2.15 Kijia cha pamoja cha kugeuka kushoto.....	15
2.16 Vijia vilivyotengwa.....	15
2.17 Matumizi ya jumla ya kijia.....	15
2.18 Vijia vya baiskeli na alama za njia ya miguu.....	16
2.19 Taa za baiskeli na wanaotembea.....	17
2.20 Wanaotembea waliolemaa macho.....	17
2.21 Mikingamo.....	17
2.22 Magari ya dharura.....	18
2.23 Mabasi ya shule.....	19
2.24 Maegesho.....	20
2.25 Ni marufuku kuegesha.....	20
2.26 Kukaribia magari yaliyosimama Sheria ya lowa ya Kuendelea Mbele au Kupunguza Kasi.....	21
2.27 Ondoa gari barabarani unapopata ajali.....	21

## **SURA YA 3: KUJITAYARISHA KUENDESHA GARI..... 22**

3.1 Kutunza gari lako.....	22
3.2 Kurekebisha viti na vioo.....	24
3.3 Mifumo mahiri ya usaidizi kwa dereva.....	25
3.4 Kufahamu maeneo yasiyoonekana vizuri.....	33
3.5 Mikanda na vizuizi vya watoto.....	33

3.6 Kufunga vifaa vilegevu.....	35
3.7 Kuondoa vivurugaji mawazo.....	35
3.8 Pombe na dawa za kulevya.....	36
3.9 Kuendesha gari ukisinzia.....	36
3.10 Kujitayarisha kwa safari barbarani - lowa 511.....	37

## **SURA YA 4: UJUZI WA MSINGI WA KUENDESHA GARI..... 38**

4.1 Kuwasha gari.....	38
4.2 Kubadilisha gia.....	38
4.3 Kukanyaga mafuta.....	39
4.4 Kufunga breki na kusimamisha gari.....	39
4.5 Kasi inayofaa.....	41
4.6 Kuzungusha usukani.....	41
4.7 Kurudi nyuma.....	42
4.8 Mbinu bora za kugeuza gari.....	42
4.9 Kubadilisha vijia.....	43
4.10 Kupita gari.....	44
4.11 Kuendesha gari kwa kupunguza hatari.....	46
4.12 Kuendesha gari salama kwenye msongamano.....	47
4.13 Kuwasiliana - taa za mbele, honi na taa za dharura.....	48

## **SURA YA 5: KUTUMIA UJUZI WAKO WA KUENDESHA GARI..... 50**

5.1 Mikingamo.....	50
5.2 Kuendesha gari kwenye barabara kuu na za juu.....	51
5.3 Mikingamo ya kupunguza migongano.....	52
5.4 Kuacha baraste ya almasi.....	53
5.5 Mizunguko.....	54
5.6 Kuendesha gari kwenye barabara ya kijijini/ changarawe.....	55
5.7 Kuendesha gari usiku.....	56
5.8 Mbawala na wanyama wengine.....	57
5.9 Kushiriki barabara na malori makubwa.....	57
5.10 Kushiriki barabara na pikipiki.....	58
5.11 Kushiriki barabara na baiskeli na wanaotembea.....	58
5.12 Magari yaliyofungwa siku yenye joto.....	59
5.13 Kuendesha gari kwenye hali mbaya ya hewa.....	59
5.14 Dharura za vifaa kuacha kufanya kazi.....	62
5.15 Kuhusika kwenye ajali.....	63
5.16 Mazungumzo na mamlaka ya utekelezaji sheria.....	64



## SURA YA 1

# LESENI YAKO YA DEREVA

---

### 1.1 JE, NI NANI ANAYEHITAJI LESENI YA DEREVA YA IOWA?

Katika jimbo la Iowa, yeyote anayeendesha gari, pikipiki au baiskeli moto kwenye barabara za umma anahitajika kuwa na kibali au leseni. Unasemekana kuwa mkazi wa Iowa kwa madhumuni ya leseni ya dereva ikiwa umefanya angalau moja ya yafuatayo:

- Umesajiliwa kupiga kura katika jimbo hili.
- Umemwandikisha mtoto wako katika shule ya umma ya Iowa.
- Umekubali kazi ya kudumu katika jimbo la Iowa.
- Umeishi Iowa mfululizo kwa siku 30.
- Umewasilisha ondoleo la kodi ya shamba au ondoleo la kodi ya jeshi kwa mali katika jimbo la Iowa.
- Unapokea msaada wa umma kutoka katika jimbo la Iowa.


HUHITAJI leseni ya dereva ikiwa wewe ni:

- Kuendesha gari la jeshi ukiwa kwenye kazi na Majeshi ya Marekani.
- Kuendesha vifaa vya shamba kati ya shamba la nyumbani na ardhi yoyote ya kilimo iliyo karibu au shughuli za shamba ndani ya fmali mbili.
- Kuendesha gari kwa leseni ya sasa kutoka kwenye jimbo la nyumbani au nchi yako huku Iowa ikiwa kama mgeni au mwanafunzi.



## TEMBELEA IOWADOT.GOV ILI UPATE MAELEZO KUHUSU:

- ✓ Wakato wa kusajili tena leseni yako na jinsi ya kufanya hivyo.
- ✓ Mpango wa Leseni ya Dereva Aliyefuzu (kwa madereva wa chini ya umri wa miaka 18).
- ✓ Kufanya jaribio la ufahamu nyumbani au shuleni (Skip the Trip)
- ✓ Aina maalum za leseni za dereva kama vile leseni za baiskeli moto na CDL.



Soma mtandaoni pamoja na jaribio letu la utendaji:

[www.iowadot.gov/mvd/driverslicense/manuals-and-practice-tests](http://www.iowadot.gov/mvd/driverslicense/manuals-and-practice-tests)

## 1.2 KUBEBA LESENI NA BIMA YAKO

Unapaswa kuwa na leseni au kibali chako wakati wote unapoendesha gari. Madereva wa magari yaliyosajiliwa lowa lazima pia wabebe kadi ya bima (iliyochapishwa au ya elektroniki) ili kuthibitisha bijima ya dhima. Kukosa kufanya hivyo kunaweza kusababisha kutozwa faini na uwezekano wa gari kukamatwa.

## 1.3 UCHUNGUZI NA VIPIMO VYA AFYA VINAVYOHITAJIKA

Unapotuma ombi la leseni ya gari, utahitajika kufanya mambo yafuatayo:

- Uchunguzi kamili wa macho.
- Kupita jaribio la ufahamu.
- Kuonyesha kwamba umekamilisha kwa ufanisi kozi ya elimu ya dereva iliyoidhinishwa na lowa (ikiwa una umri wa chini ya miaka 18).
- Kupita jaribio la kuendesha gari (hakuhitajiki ikiwa unathibitisha matakwa ya kozi ya elimu ya dereva).



## SURA YA 2

# ALAMA NA SHERIA ZA BARABARANI

## 2.1 ALAMA ZA BARABARANI

Alama za barabarani zinashauri kuhusu sheria za barabarani, hatari, eneo, maelekezo na mahali huduma zinapatikana. Umbo na rangi ya ishara za barabarani hutoa vidokezo kuhusu aina ya taarifa zinazotoa.

### RANGI WASTANI

#### NYEKUNDU

Simama, achia njia, au fanya kile ambacho kinaonyeshwa kwenye alama.

#### KIJANI

Maelekezo. Hubainisha mahali, au umbali wa mahali kutoka pale ulipo.

#### SAMAWATI

Huduma kwa wasafiri. Hukuelekeza mahali kama vile maeneo ya kupumzikia, maeneo ya watalii, hospitali, lojingi, vituo vya mafuta, mikahawa na vivutio vya watalii.

#### MANJANO

Onyo la jumla.

#### MANJANO KIJANI YA KUAKISI MWANGA

Alama za kuonya za wanaotembea, baiskeli na shule.

#### NYEUPE

Udhibiti. Hutoa taarifa kuhusu sheria na amri za kutekelezwa.

#### MACHUNGWA

Maonyo ya kazi barabarani, udhibiti wa magari wa muda mfupi na ukarabati. Hakikisha kuwa unatahadhari vikomo vya kasi vinavyobadilika na wafanyakazi barabarani.

#### HUDHURUNGI

Maeneo ya kuvutia ya burudani na utamaduni. Hutoa maelekezo ya maeneo ya historia, mbuga, au maeneo ya burudani.

#### WARIDI YA KUAKISI MWANGA

Alama za onyo na mwongozo kwa udhibiti wa ajali kama vile uondoaji wa mgongano, vifusi, n.k.

## MAUMBO WASTANI

**PEMBENNE**

Umbo linawekwa kwa alama ya kusimama pekee. Simama kabisa kwenye mkingamo unaodhibitiwa na alama hii.

**PEMBETATU SAWA**

Achia njia.

**BENDERA**

Alama hii itakuwa upande wa kushoto kwa barabara. Hukuonya kuhusu eneo lislilo la kupita.

**ALMASI**

Onyo. Hukutahadharisha kuhusu hatari maalum za barabara. Maneno au picha kwenye alama zitakuonyesha sababu ya kuhitaji kupunguza kasi au kutahadhari zaidi.

**MSTATILI**

Hutumiwa kwa alama za udhibiti, mwongozo na kuonya.

**PEMBETANO**

Kivuko cha shule. Alama zinaonyesha maeneo ya shule na vivuko vya shule.

**MSALABA**

Alama za kivuko cha reli zinawekwa katika kila kivuko. Alama ya nambari chini ya misalaba inaonyesha idadi ya reli unazopaswa kuvuka.

**DUARA**

Kivuko cha reli mbele.

## 2.2 ALAMA ZA UDHIBITI

Alama hizi zinatoa taarifa kuhusu sheria za maelekezo ya magari, matumizi ya vijia, kugeuka, kasi, kugesha na hali nyingine maalum. Alama nyingine za udhibiti zina duara nyekundu yenye fyekeo nyekundu kwenye ishara. Hizi zinaonyesha kuwa huwezi kufanya kitu; kwa mfano, hakuna kugeuka kushoto, hakuna kugeuka kulia, au hakuna mgeuko wa U.



### ALAMA ZA KIKOMO CHA KASI

Alama za kikomo cha kasi zinaonyesha kasi salama ya juu zaidi au chini zaidi inayoruhusiwa. Vikomo vya kasi ya juu zaidi ni vya hali bora za kuendesha gari. Wakati mwingine lazima upunguze kasi yako wakati hali zinahitaji, kama vile wakati barabara ni telezi (wakati wa mvua au theluji) au ni vigumu kuona vizuri barabarani (wakati wa ukungu). Baadhi ya barabara za kasi ya juu zina vikomo vya kasi ya chini. Ikiwa kasi hii ya chini ni ya haraka sana kwako, unapaswa kufuata njia nyingine.




### ALAMA YA KUACHIA NJIA

Alama ya kuachia njia inamaanisha lazima upunguze kasi na uachie njia magari kwenye mkingamo unaovuka au barabara unayoingia.



### BARABARA KUU ILIYOGAWANYWA

Barabara iliyo mbele imegawanywa. Alama hii inaelekeza magari karibu na kisiwa au kizuizi.



### ALAMA ZA KUDHIBITI VIJIA

Alama hizi huonyesha mahali unapoweza kuenda na unapoweza kugeuka, na mara nyingi hutumia ishara ya mshale. Alama ziko kwenye barabara au zinaning'inia juu ya barabara. Wakati mwingine mishale mieupe inaweza pia kupakwa barabarani.



### BARABARA YA UPANDE MMOJA

Magari yanaelekea tu upande wa mshale.



### ALAMA YA NI MARUFUKU KUINGIA

Utaona alama hii kwenye uwazi wa njia usiopaswa kuingia. Utazona kwenye njia za kutoka, katika vipito vya reli kwenye barabara zilizogawanywa na kwenye maeneo mbalimbali kwenye barabara za upande mmoja.



### ALAMA ZA NI MARUFUKU KUPITA

Alama hizi huonyesha mahali ambapo si salama kupita gari jingine. Alama ya eneo ambalo ni marufuku kupita inapatikana mwanzo wa eneo ambalo ni marufuku kupita. Maeneo ya kupita yanategemea umbali ambao unaweza kuona mbele. Pale ambapo unaruhusiwa kupita, unaweza kufanya hivyo tu ikiwa ni salama. Alama za njia ya miguu za eneo ambalo ni marufuku kupita zimefafanuliwa kwenye ukurasa wa 44.



### NJIA ISIYOFAA

Ulifanya mgeuko usiofaa na umeingia kwenye kijia cha magari yanayokuja. Ondoa gari lako sehemu ya barabara inayopita magari na usimame na kugeuza gari haraka na kwa usalama iwezekanavyo.



### ALAMA YA KUSIMAMA

Alama ya kusimama inamaanisha kwamba lazima usimame kikamilifu na usubiri hadi magari na wanaotembea ambao wanavuka waishe kabla ya kuendelea na safari. Simama kwenye mstari wa kusimama ikiwa upo. Ikihitajika, unaweza kusonga mbele hadi kwenye alama ya kusimama au ukingo wa mkingamo na kisha uendelee wakati ni salama kufanya hivyo



## 2.3 ALAMA ZA KUONYA

Alama za kuonya ni za manjano zenye herufi au ishara nyeusi na nyingi zina umbo la almasi. Alama hizi zinakuonya kupunguza kasi na kujitayarisha kusimama ikihitajika; tukio maalum au hatari iko mbele. Baadhi ya alama maarufu za kuonya zimeonyeshwa hapa chini.



**MKINGAMO/NJIA PANDA**  
Kuna barabara nyingine mbele ambayo inavuka barabara unayofuata. Kuwa makini kwa magari yanayovuka kwenye njia yako.



**KIJIA KINAISHA**  
Vijia viwili vya magari vitakuwa kijia kimoja cha magari hivi karibuni. Lazima magari yaachie njia yanapojiunga na mengine.



**MPINDO WA POLEPOLE**  
Barabara iliyo mbel inapinda polepole. Jitayarisha kwa mabadiliko ya mwelekeo.



**TAA MBELE**  
Alama hizi hutumika kwenye barabara zilizo na vikomo vya kasi za juu. Kuwa tayari kwa mkingamo na taa ya kusimama.



**MASHINE ZA SHAMBANI**  
Tahadhari vifaa vya shambani vinavyoendeshwa polepole kwenye barabara. Punguza kasi na upite polepole.



**TELEZI WAKATI WA UNYEVU**  
Barabara iliyopo mbele inakuwa telezi wakati kuna unyevu. Punguza kasi wakati wa hali hizi.



**MAGARI YANAYOUNGANA**  
Ikiwa uko kwenye barabara kuu na uone alama hii, kuwa tayari kwa magari mengine kuingia kwenye kijia chako.



**WANAOTEMBEA WANAVUKA**  
Tahadhari watu ambao wanaweza kutembea au kukimbia mbele ya gari lako.




**ALAMA YA CHEVRONI**  
Hutumiwa mbali na alama za mpindo wakati kuna haja ya kuteka makini ya badiliko la mwelekeo wa barabara.



**MAGARI YA PANDE MBILI**  
Kaa kulia kwa sababu unaondoka kwenye barabara ya upande mmoja na kuingia barabara ya pande mbili.



**MBAWALA ANAVUKA**  
Huenda mbawala anajaribu kuvuka barabara katika eneo hilo. Punguza kasi na uangalie kwa makini.



**KASI YA NJIA YA KUTOKA**  
Kasi inayopendekezwa kwenye njia ya kutoka.



**BARABARA KUU ILIYOGAWANYWA INAANZA**  
Unakaribia sehemu ambapo magari ya pande mbili yatagawanywa kwa mstari wa katikati.



**KILIMA**  
Alama hii ni onyo kwa magari yote kwamba barabara iliyo mbele inaelekea kwenye kilima. Unapaswa kuangalia breki zako kabla ya kuteremka mlimani.



**KIVUKO CHA SHULE CHA MAPEMA**  
Unakaribia eneo la shule lililo na kivuko. Tahadhari watoto na kivuko cha shule kilichotiwa alama. Rangi ya alama hii inaweza kuwa manjano.

AHEAD

OR

200 FT

OR

200 FEET



**BARABARA KUU INAISHA**  
Magari ya pande mbili hayatagawanywa tena kwa mstari wa katikati. Tahadhari magari yanayokuja.



**MKINGAMO WA T UKO MBELE**  
Barabara unayofuata hainyoki mbele. Jitayarisha kugeuka kulia au kushoto.




**GARI LINALOKOKOTWA NA FARASI**  
Tahadhari kwa magari yanayoenda polepole yanayokokotwa na farasi wenye barabara. Punguza kasi na upite polepole



**KITUO CHA MABASI YA SHULE MBELE**  
Unakaribia eneo ambapo basi la shule lililosimama litachukua au kuwashusha abiria. Tahadhari watoto. Jitayarisha kusimama.

## 2.4 ALAMA YA GARI LINALOENDESHA POLEPOLE

Pembetatu ya machungwa inayoakisi nyuma ya gari inamaanisha linasafiri kwa mwendo wa maili 35 kwa saa au kidogo. Huenda ukaona alama hii kwenye kifaa cha kukarabati barabara, magari ya mashamba, au yanayokokotwa na farasi.



## 2.5 ALAMA ZA MWONGOZO

Alama za mwongozo huonyesha maelekezo na umbali wa maeneo mbalimbali, au maeneo kama vile majiji, viwanja vya ndege, mipaka ya majimbo; au sehemu za kuvutia kama vile mbuga za taifa, maeneo ya historia au makavazi. Vialamishi vya maili vinaonyesha idadi ya maili kutoka mahali ambapo njia ya Intersate iliingia katika jimbo unaloelekea. Zinaweza kutumiwa kukokotoa umbali wako kutoka njia ya kutoka au unakoenda na kukupa eneo halisi wakati wa dharura.



## 2.6 ALAMA ZA HUDUMA

Alama za huduma zinaonyesha eneo la huduma mbalimbali; kama vile maeneo ya kupumzikia, vituo vya mafuta, viwanja vya kambi, au hospitali.



## 2.7 ALAMA ZA NJIA

Umbo la alama ya njia linabainisha aina ya barabara yenyewe - majimbo mbalimbali; barabara kuu ya Marekani, njia ya Iowa, barabara ya mashabani, n.k. Wakati wa safari, fuata alama ili usalie kwenye njia yako.



## 2.8 TAA ZA BARABARNI

Mbali na taa za barabarani, udhibiti w taa unaweza kutekelezwa na mamlaka ya sheria, watumishi wa barabara kuu au walinzi wa kivuko cha shule. Lazima ufuate maelekezo kutoka kwa watu hawa.



Taa wastani ya magari

### Nyekundu thabiti

Simama kikamilifu.

### Nyekundu inayomweka

Ichukulia sawa na alama ya kusimama.

### Manjano thabiti

Usiingie kwenye mkingamo ikiwa unaweza kusimama bila tatizo. Ikiwa huwezi kusimama salama, endelea kupitia kwenye mkingamo kwa tahadhari.

### Manjano inayomweka

Endelea kwa tahadhari. Achia njia magari na wanaotembea na uendelee ikiwa salama.

### Kijani thabiti

Nenda, lakini tu wakati mkingamo hauna magari. Achia njia magari na wanaotembea katika mkingamo. Wakati taa inabadilika, huenda magari yakapatikana kwenye mkingamo, na lazima uyape muda yaishe.



Taa ya mshale mbele

### Mshale mwekundu thabiti

Madereva wanaogeuka kushoto au kulia lazima wasimame.

### Mshale wa manjano thabiti

Taa ya kugeuka kushoto au kulia inakaribia kubadilika kuwa nyekundu. Usiingie kwenye mkingamo ikiwa unaweza kusimama bila tatizo. Kamilisha mgeuko wako wa kushoto au kulia ikiwa tayari umo ndani ya mkingamo.

### Mshale wa manjano inayomweka

Achia njia magari yanayokuja na wanaotembea; kisha geuka kushoto ukiendelea kwa tahadhari. Magari yanayokuja yana taa ya kijani.

### Mshale wa kijani thabiti

Madereva wanaweza kuendelea na mgeuko wa kushoto au kulia. Lazima magari yanayokuja yasimame. Usiende moja kwa moja. Endesha gari tu upande wa mshale. Achia njia magari mengine na wanaotembea tayari walio katika mkingamo.

## 2.9 VIVUKO VYA RELI

Tumia tahadhari kwenye vivuko vya reli na usiwahi kusimamisha gari lako kwenye reli. Magarimoshi hayawezi kusimama haraka.

Ishara za kuonya mapema na alama za njia ya wanaotemba hubainisha kivuko cha reli mbele. Unapokaribia reli, ondoa vitekaji nyara makini, teremsha madirisha yako na uzime muziki wako. **Angalia kielelezo cha 2.1 kwa alama maarufu za kivuko na taa za reli.**

Vivuko vya reli vya juu vina jina la reli na nambari ya kupiga simu iliyochapishwa endapo kuna dharura. Ukifahamu kuhusu kasoro ya taa au hali nyingine ya hatari (kama vile gari lililokwama, kitekaji nyaraka makini, au kuharibika kwa reli), piga simu nambari iliyochapishwa ili kuarifu reli inayofaa (*angalia picha ya kulia chini ya alama ya ENS*).

### VIVUKO VYA RELI VINAVYOLINDWA MARA KWA MARA

Vivuko vya reli vinavyolindwa mara kwa mara vina taa na/au malango. Ikiwa taa zinamweka au malango yako chini, inamaanisha garimoshi linakuja. Tii taa hizi za kuonya kila wakati. Usivuke wakati taa zinamweka wala kujaribu kuenda karibu na lango.

### VIVUKO VYA RELI VINAVYOLINDWA KIASI

Vivuko vya reli vinavyolindwa kiasi havina taa wala malango. Vitatia alama tu kwa alama ya msalaba na alama ya kusimama au kuachia njia. Kwenye kivuko cha aina hii, punguza kasi na uangali ikiwa garimoshi laja. Usitegemee taa wala lango lolote na utarajie garimoshi kila wakati.



Alama za Kivuko Kiasi

### UNAHITAJIKA KUSIMAMA

Magari yote ya shule, mabasi ya shule za gharama nafuu, madereva wanaowabeba abiria ya kukodisha (kama vile Uber au Lyft) na magari yote yanayohitajika kuwa na mabango ya nyenzo hatari, lazima yasimame ndani ya futi 15 hadi 50 wa reli kabla ya kuvuka. Ikiwa afisa wa polisi au taa ya magari ya barabara kuu inaelekeza magari ya barabara kuu kuendelea, si lazima usimame. Pia si lazima usimame ikiwa kivuko kimetiwa alama ya "EXEMPT".

## FANYA MAAMUZI SALAMA

*Chanzo: Operation Lifesaver*

### Vuka Kihalali na Salama

- Sehemu salama na halali pekee kwa yeyote kuvuka reli ni kwenye vivuko maalum.
- Tii alama na taa za kuonya.
- Si reli zote za garimoshi zilizo na malango. Tahadhari alama za kuonya za mapema na za njia ya miguu zikionyesha kivuko cha reli mbele.
- Magari ya reli yana mistari ya kuakisi ili kuboresha mwonekano wao usiku na katika mazingira mengine ya mwonekano, kama vile mvua, theluji, au ukungu. Tahadhari hizi wakati hali zinaweza kutatiza kuona garimoshi.
- Angalia ikiwa kuna garimoshi kabla ya kuendelea.

### Subiri, Angalia Njia Zote Mbili

- Tarajia garimoshi kila wakati.
- Magarimoshi yanaweza kuwa karibu na yakisafiri haraka kuliko inavyoonekana na yanaweza kukanyaga reli yoyote wakati wowote.
- Reli nyingi zinaweza kumaanisha magari moshi mengi. Hakikisha kuwa unaweza kuona vizuri chini ya reli katika pande zote kabla ya kuendelea.
- Epuka kuvuka wakati taa zinamweka au malango yako chini. Usiwahi kujaribu kushinda garimoshi

### Epuka Kukwama

- Kabla ya kuvuka, hakikisha kuwa unaweza kukaa mbali na reli. Fahamu kwamba magari moshi ni mapana kuliko reli.
- Unaposimamishwa, acha angalau futi 15 kati ya sehemu ya mbele na nyuma ya gari lako na reli ya karibu.
- Epuka kubadilisha gia unapovuka.

### Toka, Nenda, Tafuta Alama ya Samawati na Nyeupe

- Ikiwa gari lako limekwama kwenye kivuko, mwambie kila mtu ashuke na kukaa mbali mara moja, hata ikiwa huoni garimoshi.
- Piga simu nambari iliyo kwenye alama ya samawati na nyeupe ya Emergency Notification System (ENS). Shiriki nambari ya kitambulisho ya kivuko na msimamizi.



Alama ya ENS

- Ikiwa hakuna alama, pigia 911.

## Kielelezo cha 2.1: Operation Lifesaver - Jua Alama na Taa

**JUA ALAMA NA TAA****RELI NYINGI**

Reli nyingi zipo. Reli nyingi zinaweza kumaanisha magarimoshi mengi. Subiri hadi uone vizuri chini ya reli pande zote kabla ya kuendelea.

**MSALABA**


ACHIA NJIA ikiwa garimoshi laja. Magarimoshi yana haki ya kupita siku zote.

**TAA NYEKUNDU ZINAZOMWEKA**

SIMAMA wakati zinamweka. USIENDELEE hadi zimweke ukishaanza kwenye reli, endelea.

**KUTEREMSHA MALANGO NA TAA NYEKUNDU ZINAZOMWEKA**

Garimoshi laja (hata kama bado hulioni). Usiendeleo hadi taa zizimike na lango kupanda juu. Ni haramu na hatari kuenda karibu na malango yaliyoteremshwa.


**MFUMO WA ARIFA WAKATI WA DHARURA (ENS)**

Hii ni nambari ya simu ya kwanza ya kupiga ikiwa gari limekwama kwenye reli. KUMBUKA: Kila alama ina nambari ya simu tofauti na nambari ya kitambulisho cha eneo.

Pia tumia ENS kuripoti watu, magari au vifusi kwenye reli, alama au taa zilizoharibiwa na uwezo wa kuona ulioathiriwa.

**ALAMA ZA NJIA YA MIGUU**

RxR na mstari mweupe mpana kwenye barabara inamaanisha kuwa unakaribia kivuko cha reli. Kaa nyuma ya mstari mweupe wa kusimama unaposubiri garimoshi lipite. Hakuna mstari wa kusimama? Simama angalau futi 15 kutoka reli ya karibu.

**KIVUKO CHA UONDOAJI CHA CHINI**

Kivuko kilichoinuliwa kipo mbele. Ukiendesha chochote chini kwenye ardhi – kama lowboy, basi, gari la michezo au trela – uko kwenye hatari ya kuning'inia kwenye reli. Usiendeleo hadi ujue kuwa gari lako litakaa mbali na reli.

**ONYO LA MAPEMA**

Punguza kasi, angalia, sikiliza na ujitayarisha kusimama. Kwa kawaida, hii ni alama ya kwanza unayoona wakati unapokaribia kivuko cha reli.



Chanzo: Operation Lifesaver: [https://oli.org/sites/default/files/2021-01/OLI\\_Brochure\\_All\\_Drivers\\_WEB\\_version.pdf](https://oli.org/sites/default/files/2021-01/OLI_Brochure_All_Drivers_WEB_version.pdf)

## 2.10 MAENEO YA KAZI

Vifaa vya kudhibit magari kama vile bodi za mishale, taa za muda mfupi za magari, wadhibiti wa magari na vifaa vya kuonya na kutahadharisha vinaongezwa kwenye maeneo ya kazi ili kuwafahamisha madereva kuhusu hali tofauti. Alama nyingi katika maeneo ya kazi zina umbo la almasi, ingawa alama chache ni za mstatili. Machungwa ni rangi ya msingi ya alama hizi na vifaa vya kuonya.

Vifaa vya kudhibiti magari na alama hutumiwa kuweka alama kwenye maeneo ya ujenzi, ukarabati, uchunguzi na kazi za huduma. Hivi husaidia madereva na wanaotembea kupita salama eneo la kazi huku vikiwalinda wafanyakazi barabarani. **Tahadhari na uendeshe gari kwa uangalifu kwa kuwa faini zinaweza kuwa maradufu katika maeneo ya kazi.**

Maeneo ya kazi yanaweza kuwa hatari na wafanyakazi barabarani wanakutegemea kuwalinda:

**REKEBISHA KASI YAKO KULINGANA NA HALI ZA BARABARANI.**

**TII MAAGIZO YOTE YALIYOTOLEWA NA ALAMA, TAA ZA BARABARANI NA WADHIBITI WA MAGARI.**

**ONGEZA UMBALI WA KUFUATA.**

**WEKA MAKINI YAKO YOTE KWENYE UENDESHAJI GARI.**



## BODI ZA MISHALE

Paneli kubwa za mishale inayomweka kwa kawaida hutumiwa wakati kijia au kijia cha dharura kimefungwa.



## WADHIBITI WA MAGARI

Watu walio na kafi za kusimama/kupunguza kasi husaidia magari katika maeneo ya kazi. Fuata maagizo yao. Wanapaswa kuvalia vesti, mashati au majaketi ya manjano kijani ya kuakisi mwanga. Kwa kawaida hutumia alama za simama/punguza kasi. Bendera nyekundu zinaweza kutumiwa mara mojamoja.



## VIFAA VYA KUONYA NA KUTAHADHARISHA

Vizuizi, paneli za wima, mapipa, pia na vialamishi vya mabomba ni vifaa maarufu sana vinavyotumiwa kuwatahadhrisha

madereva kuhusu hali zisizo za kawaida na zinazoweza kuwa hatari na kuwaongoza madereva kupita salama katika eneo la kazi.



### Kielelezo cha 2.2: Alama za kudhibiti vijia



Barabara ya upande mmoja




Barabara ya pande mbili

### Kielelezo cha 2.3: Mistari ya kuachia njia



### Kielelezo cha 2.4: Kivukomilia, mistari ya kusimama na alama za mishale ya kuelekeza




A Mistari ya kusimama

B Alama za mishale ya kuelekeza

C Aina tofauti za vivukomilia

### Kielelezo cha 2.5: Vijia vya kupindukia



## 2.11 ALAMA ZA NJIA YA MIGUU NA VIDHIBITI VINGINE VYA VIJIA

Alama za njia ya miguu husaidia kuelekeza na kudhibiti magari kama tu alama za barabara kuu. Utazipata pekee au hutumiwa pamoja na alama na taa za barabarani. Mistari mieupe inatenganisha magari yanayoenda upande mmoja. Mistari ya manjano inatenganisha magari yanayoenda pande tofauti.

Kwenye barabara za pande mbili utaona mstari wa manjano thabiti ulio na mstari uliojigawa kando katika sehemu nyingine. Ni marufuku kupita upande ulio na mstari wa manjano thabiti. Magari yaliyo upande ulio na mstari uliojigawa yanaweza kupita wakati ni salama kufanya hivyo.

## 2.12 MISTARI YA KUACHIA NJIA

Mistari ya kuachia njia ina safu ya pembetatu nyeupe thabiti zinazoashiria magari yanayokuja. Mistari hii inaenda hadi kijia cha kusafiria kuonyesha mahali ambapo magari yanapaswa kuachia njia kwa mujibu wa alama ya “Achia Njia” au alama ya “Achia Njia Hapa Wanaotembea”.

## 2.13 VIVUKOMILIA, MISTARI YA KUSIMAMA NA ALAMA ZA MISHALE YA KUELEKEZA


Unapohitajika kusimama kwa sababu ya alama au taa, lazima usimame kabla ya gari lako kufikia mstari wa kusimama, au kivukomilia ikiwa kipo. Vivukomilia hubainisha eneo ambalo wanaotembea wako ili kuvuka barabara. Lazima uachie njia wanaotembea walio au wanaokaribia kuingia kwenye kivukomilia. Si vivukomilia vyote vilivyotiwa alama. Tahadhari wanaotembea wakati wa kuvuka mikingamo ambayo haina vivukomilia vilivyobainishwa.

Alama maalum za mishale zinaweza kuwepo na zinapotumiwa huonyesha miondoko inayoruhusiwa au inayohitajika wakati unapoelekea kwenye kijia hicho.

## 2.14 VIJIA VYA KUPINDUKIA

Baadhi ya vijia vya kusafiria vimeundwa ili kubeba magari upande mmoja nyakati fulani na upande mwingine nyakati nyingine. Vijia hivi kwa kawaida vimetiwa alama kwa mistari ya manjano iliyojigawa maradufu. Kabla hujaanza kuendesha gari kwayo, thibitisha vijia unavyoweza kutumia wakati huo. Huenda kukawa na alama zilizochapishwa kando ya barabara au juu. Wakati mwingine taa maalum hutumika. Mshale wa kijani unamaanisha unaweza kutumia kijia kilicho chini yake; “X” nyekundu inamaanisha huwezi. “X” ya manjano inayomweka inamaanisha kijia ni cha kugeukia pekee. “X” ya manjano thabiti inamaanisha kwamba matumizi ya kijia yanabadilika na unapaswa kuondoka kwacho pindi tu inapokuwa salama kufanya hivyo.

### Kielelezo cha 2.6: Kijia cha pamoja cha kugeuka kushoto



### Kielelezo cha 2.7: Alama ya kijia kilichotengwa

Katika mfano huu, kijia kimetengewa magari ya usafiri wa umma (HOV) yanayobeba watu wawili au zaidi.

## 2.15 KIJIA CHA PAMOJA CHA KUGEUKA KUSHOTO

Vijia vya pamoja vya kugeuka kushoto vimetengewa magari yanayogeuka kushoto kutoka upande wowote. Kwenye njia ya miguu, mishale ya kugeuka kushoto kwa magari ya upande mmoja hubadilishana na mishale ya kushoto kwa magari yanayokuja kutoka upande mwingine. Vijia hivi vimetiwa alama kila upande kwa manjano thabiti na mstari wa manjano uliojigawa. Magari yanaweza kuingia na kusimama kwenye kijia kabla ya kugeuka kushoto, lakini kijia hakiwezi kutumiwa kupita.


## 2.16 VIJIA VILIVYOTENGWA

Kwenye barabara mbalimbali kijia kimoja au zaidi vinaweza kutengewa magari maalum. Vijia vilivyotengwa vimetiwa alama zikibainisha kuwa kijia kimetengewa matumizi maalum na mara nyingi vimewekwa almasi upande wa barabara na/au kupakwa rangi juu ya barabara. Usisafiri kwenye moja ya vijia hivi isipokuwa uwe unaendesha gari la aina hiyo.

## 2.17 MATUMIZI YA JUMLA YA KIJIA

- Kwenye barabara yenye vijia viwili au zaidi vinavyoelekea upande mmoja, kijia cha kushoto hutumika kupita kwa jumla. Kwenye barabara yenye vijia vitatu au zaidi kaa kwenye kijia cha kulia au katikati isipokuwa kupita. Ikiwa kuna magari mengi yanayoingia, ni vizuri utumie kijia cha katikati.
- Isipokuwa uagizwe kufanya hivyo na kifaa cha kudhibiti magari au afisa, usiwahi kuendesha gari kwenye kijia cha dharura cha barabara.
- Usiwahi kupitia kwenye kijia cha dharura, kiwe kina njia ya miguu au hakina. Madereva wengine hawatakutarajia kuwepo hapo na huenda wakaondoka kwenye barabara bila kuangalia.
- Pale ambapo hapana ishara au alama za kijia kudhibiti ugeukaji, unapaswa kugeukia kwenye kijia kilicho karibu na upande unaotaka kuenda na uingie katika kijia kilicho karibu na kile ulichotoka. (*Angalia kielelezo cha 2.8*)
- Unapofanya migeuko, nenda kutoka kijia kimoja hadi kingine moja kwa moja inavyowezekana bila kuvuka mistari ya vijia au kuhitilafiana na magari. Pindi unapokamilisha kugeuka, unaweza kuhamia kijia kingine ukihitaji kufanya hivyo.

**Kielelezo cha 2.8: Unapofanya migeuko, kaa kwenye kijia chako na ugeukie kwenye kijia kilicho karibu na kile ulichotoka.**



## 2.18 VIJIA VYA BAISKELI NA ALAMA ZA NJIA YA MIGUU

### VIJIA VYA BAISKELI

Vijia vya baiskeli ni sehemu za barabara ambazo zimekusudiwa matumizi ya waendeshaji wa baiskeli na zimetwa alama kwa mistari mieupe thabiti, pamoja na alama na ishara za njia ya baiskeli.

- Vijia vingine vya baiskeli vinaweza kutenganishwa zaidi na magari kupitia matumizi ya mistari mieupe iliyojigawa, vizuio, mabango au vyungu vya mimea.
- Vijia vya baiskeli vinaweza kujazwa rangi ya kijani na madereva wanapaswa kuwa makini zaidi na kuangalia waendeshaji wa baiskeli kabla ya kuvuka njia ya miguu ya kijani. Madereva hawapaswi kusimama kwenye njia ya miguu ya kijani. (Angalia kielelezo cha 2.9)
- Madereva wanaweza tu kuendesha gari katika vijia vya baiskeli wakati wanapofanya migeuko na lazima wawe waangalie kwa makini kando na nyuma ya gari ikiwa kuna waendeshaji wa baiskeli na kuvuka kwa uangalifu.

### ALAMA ZA VIJIA ZA PAMOJA

Alama za vijia vya miguu za pamoja, pia huitwa "sharrows" huwatahadharisha madereva kuhusu kuwepo kwa waendeshaji baiskeli, huhimiza madereva kuwapita salama waendeshaji baiskeli na kupunguza matukio ya kuendesha baiskeli kwenye njia isiyofaa na uwezekano wa kugonga milango. Tofauti na vijia vya baiskeli, sharrow hazibainishi sehemu maalum ya barabara kwa matumizi ya baiskeli pekee. (Angalia kielelezo cha 2.10)

### VISANDUKU VYA BAISKELI

Visanduku vya baiskeli ni alama za njia ya miguu ambazo zimewekwa ili kuruhusu waendeshaji baiskeli kuwa na njia salama ya kugeukia kwenye mkingamo wenye taa. Visanduku vya baiskeli ni kijani thabiti na vina picha ya mwendeshaji baiskeli. Vinapatikana karibu na kivukomilia na vinachukua upana mzima wa kijia cha kusafiri. (Angalia kielelezo cha 2.11)

### ISHARA YA KIGUNDUZI CHA BAISKELI


Ishara inaweza kuwekwa kwenye njia ya miguu ikionyesha nafasi bora kwa mwendeshaji basikeli kuwasha/kuchochea taa ya barabarani.




Kielelezo cha 2.9: Kijia cha baiskeli cha kijani



Kielelezo cha 2.10: Alama za vijia za pamoja



Kielelezo cha 2.11: Visanduku vya baiskeli





## 2.19 TAA ZA BAIKELI NA WANAOTEMBEA

### VIOLEZA VYA MSTATILI VYA KUMWEKA HARAKA


Violeza vya Mstatili vya Kumweka Haraka huwashwa kwa mkono na wanaotembea kwa kitufe cha kusukuma na mara nyingi hupatikana kwenye mikingamo isiyo na taa za barabarani au kwenye vivukomilia vya kati. Vinapowashwa, taa za rangi ya kaharabu humweka kwa mtindo wa haraka. Lazima madereva wasimame kwa ajili ya wanaotembea ndani ya kivukomilia na kutahadhari wanaotembea ambao wanakaribia kuingia kwenye kivukomilia kioleza kinapomweka.



Kielelezo cha 2.12: Kielezo cha mstatili kinachomweka haraka

### VIOLEZA VYA WANAOTEMBEA VYA HYBRID

Violeza vya Wanaotembea vya Hybrid huwaruhusu wanaotembea kuvuka salama barabara. Violeza hivi hutumika wakati anayetembea ameviwasha. Wakati taa zote zimezimika, madereva wanaweza kuendelea kwa tahadhari. Pindi zinapowaka, taa ya manjano ya chini inamweka na lazima madereva wapunguze kasi. Kisha taa ya manjano ya chini inakuwa thabiti na lazima madereva wajitayarishe kusimama. Kisha taa nyekundu mbili za juu zinakuwa thabiti na lazima madereva wasimame ili wanaotembea wapite. Baada ya muda mfupi, taa nyekundu mbili za juu zitaanza kumweka. Lazima madereva wasimame ikiwa bado hawajafanya hivyo na kisha wanaweza kuendelea kwa tahadhari ikiwa kivukomilia hakina watu.



Kielelezo cha 2.13: Kielezo cha wanaotembea cha hybrid

## 2.20 WANAOTEMBEA WALIOLEMAA MACHO

Ikiwa gari lako linakaribia mtu anayeongozwa na mnyama wa huduma aliyefungwa lijamu, anayetembea kwa fimbo ambayo ni nyeupe au nyeupe yenye ncha nyekundu, mtu huo anaweza kuwa na ulemavu wa macho. Tahadhari zaidi kuzuia jeraha kwa mtu huyo.

## 2.21 MIKINGAMO

### WAKATI WA KUACHIA NJIA

Wakati magari au wanaotembea wana uwezekano wa kukutana na hakuna alama wala taa za kudhibiti magari, kuna sheria zinazosema yule ambaye lazima aachie njia. Sheria hizi huwaambia madereva yule anayeenda kwanza na yule ambaye lazima asubiri katika hali tofauti barabarani. Sheria inasema yule ambaye lazima **aachie** njia; sheria **haimpi** yeyote haki ya kupita. Bila kujali yule aliye na haki ya kupita, unapaswa kufanya kila uwezalo kuzuia kugonga anayetembea au gari jingine.

Tahadhari haswa waendeshaji baiskeli. Ingawa waendeshaji baiskeli na madereva lazima washiriki haki na majukumu sawa ya kutumia barabara, madereva wanapaswa kutambua kuwa waendeshaji baiskeli wako kwenye hatari sana wakati wa migongano. Kwa hivyo, madereva wanapaswa kutumia ujuzi bora wa kuendesha gari kwa kupunguza hatari ili kuepuka migongano na waendeshaji baiskeli. Kuwa tayari kuachia njia, hata wakati waendeshaji baiskeli wanapaswa kukuachia. Hawana utetezi dhidi ya gari, hivyo ni jukumu lako kama dereva kuwatahadhari.



**KUKOSA KUACHIA NJIA NI CHANZO #1 CHA VIFO VINAVYOHUSIANA NA MAGARI BARABARANI KATIKA JIMBO LA IOWA.**

## MIKINGAMO INAYODHIBITIWA (ILİYOTIWA ALAMA)


Sheria za haki ya kupita zinatumiwa kwenye mikingamo:

- Lazima uachie njia wakati unataka kugeuka kulia baada ya kusimama kwenye taa nyekundu. Migeuko ya kulia kwenye taa nyekundu inaruhusiwa isipokuwa kuwe na alama inayoipiga marufuku.
- Madereva wanaovuka njia ya miguu, wanaoingia au kutoka kwenye njia ya binafsi, kichocho au maegesho lazima waachie njia wanaotembea. Ni haramu kuendesha gari kwenye njia ya miguu isipokuwa kuivuka.
- Madereva wanaogeuka kushoto lazima waachie njia magari yanayokuja ambayo yanafululiza moja kwa moja. (Angalia kielelezo cha 2.14a)
- Kwenye kituo cha barabara nne, dereva anayefika kwenye mkingamo wa kwanza anapaswa kuenda wa kwanza (baada ya kusimama kikamilifu). Kwa magari yanayowasili wakati mmoja, gari la upande wa kulia linaenda la kwanza. (Angalia kielelezo cha 2.14b)
- Madereva wanaoingia kwenye barabara kutoka njia ya binafsi, kichocho au kando ya barabara lazima waachie njia magari ambayo tayari yako kwenye barabara kuu.
- Lazima uachie njia au usimame kwa ajili ya wanaotembea katika vivukomilia vilivyowekwa na visivyowekwa alama.


## MIKINGAMO ISİYODHIBITIWA (ISİYOWEKWA ALAMA)

Kwenye mkingamo ambapo hapana alama ya kusimama wala taa ya barabarani, ni jukumu la madereva wote kupunguza kasi na kuenda kwa makini. Sheria hizi zote zilizo rodheshwa hapo juu zinazotumiwa kwenye mkingamo unaodhibitiwa pia zinatumiwa kwenye mkingamo usiodhibitiwa. Tahadhari zaidi inapaswa kuchukuliwa kwenye mikingamo isiyodhibitiwa.


Lazima gari jekundu liachie njia magari yanayokuja katika mifano hii.




**Kielelezo cha 2.14a: Kituo cha barabara mbili (gari la kuvuka halisimami)** - Kwa sababu gari jekundu linageuka kushoto kwenye magari, lazima gari jekundu liachie njia gari la kijani linalofululiza moja kwa moja.



**Kielelezo cha 2.14b: Kituo cha barabara nne** - Magari mawili yanawasili kwenye mkingamo kwa wakati mmoja. Dereva aliye kushoto (gari jekundu) lazima aachie njia dereva aliye kulia (gari la kijani).



**Kielelezo cha 2.14c: Kuachia njia gari linalovuka** - Lazima magari mekundu yaachie njia magari ya kijani.




**Kielelezo cha 2.14d: Mkingamo usiodhibitiwa** - Magari mawili yanawasili kwenye mkingamo kwa takribani wakati mmoja. Dereva aliye kushoto (gari jekundu) lazima aachie njia dereva aliye kulia (gari la kijani).

## 2.22 MAGARI YA DHARURA


Achia njia gari la polisi, gari la zimamoto, gari la wagonjwa, au gari jingine la dharura linalotumia king`ora au honi hewa na/au taa nyekundu au za samawati zinazomweka kwa kuchukua hatua zifuatazo:

- Egesha kwenye ukingo wa kulia wa barabara, au karibu na upande wa kulia iwezekanavyo, unapona au kusikia gari la dharura likija kutoka upande wowote.
- Ikiwa uko kwenye mkingamo (ikiwa ni pamoja na mizunguko), endesha gari kupitia kwenye mkingamo kabla hujaegesha. Hata hivyo, ikiwa uko kwenye barabara au barabara kuu iliyotenganishwa kwa kitenganishi na gari la dharura liko upande mwingine, huhitajiki kusimama.
- Kaa angalau futi 500 nyuma ya gari lolote la dharura linalotumia taa na ving`ora.


**VIJIA 3 AU VICHACHE: MAGARI YOTE LAZIMA YASIMAME**



Barabara kuu ya vijia viwili




Barabara kuu ya vijia viwili iliyo na kijia cha kugeuka katikati




Barabara kuu ya vijia vitatu

**VIJIA 4 AU ZAIDI: MAGARI YANAYOKUJA KUTOKA NYUMA LAZIMA YASIMAME**



Barabara kuu ya vijia vinne



Barabara kuu ya vijia vinne iliyo na kijia cha kugeuka katikati

**Kielelezo cha 2.15: Matukio ya basi la shule lililosimama**

**2.23 MABASI YA SHULE**

**BASI LA SHULE TUKIO LA 1**

**Unaendesha gari kwenye barabara ya vijia viwili au vitatu**

**Kufikia basi kutoka nyuma**

Ukiona taa za kuonya nyekundu au kaharabu, huruhusiwi kupita basi la shule na unapaswa kujitayarisha kusimama. Simama nyuma ya basi la shule wakati basi la shule lina simama na mkono wa kusimama unazidi kusalia juu. Usisimame karibu na futi 15 kutoka nyuma ya basi na uendelee kusimama hadi mkono wa kusimama uondolewe na basi la shule kuanza kuenda tena. Endelea kwa tahadhari.

**Kukutana na basi kutoka mbele**

Ukiona taa za kuonya za kaharabu zikimweka, lazima upunguze kasi ya gari lako kwa kasi isiyozidi maili 20 kwa saa na ujitayarisha kusimama. Simama mbele ya basi la shule wakati basi lina simama na mkono wake wa kusimama unaendelea kusalia juu. Endelea kusimama hadi mkono wa kusimama uondolewe. Endelea kwa tahadhari.

**Kukiuka sheria hii kunaweza kusababisha leseni yako kusimamishwa kwa hadi siku 180.**

**BASI LA SHULE TUKIO LA 2**

**Unaendesha gari kwenye barabara iliyo na vijia vinne au zaidi**

**Kufikia basi kutoka nyuma**

Unapokaribia kutoka nyuma, sheria ni sawa na zile za barabara ya vijia viwili au vitatu. Ukiona taa za kuonya nyekundu au kaharabu, huruhusiwi kupita basi la shule na unapaswa kujitayarisha kusimama. Simama nyuma ya basi la shule wakati basi la shule lina simama na mkono wake wa kusimama unaendelea kusalia juu. Usisimame karibu na futi 15 kutoka nyuma ya basi na uendelee kusimama hadi mkono wa kusimama uondolewe na basi la shule kuanza kuenda tena. Endelea kwa tahadhari.

**Kukutana na basi kutoka mbele**

Wakati unakutana na basi katika moja ya vijia viwili (au zaidi) vya mkabala, huhitaji kusimama, hata ikiwa basi limesimama huku taa zikimweka na mkono wa kusimama uko nje. Huu ndio wakati tu unaoweza kupita basi la shule ambalo limesimama na mkono wake wa kusimama unaendelea kusalia juu.

**Kukiuka sheria hii kunaweza kusababisha leseni yako kusimamishwa kwa hadi siku 180.**



## 2.24 MAEGESHO

Madereva wana jukumu la kuhakikisha kuwa magari yao hayawi hatari baada ya kuegeshwa. Unapoegesha gari, fuata miongozo hii.

- Egesha katika eneo lililotengwa, ikiwezekana.
- Ikiwa utalazimika kuegesha kwenye njia, egesha gari lako mbali kabisa na magari ya barabarani inapowezezekana. Ikiwa kuna kizuio, egesha ndani ya inchi 18 za kizuio au karibu.
- Egesha mbali kabisa na kijia chochote cha kusafiri ili kuepuka kuhitilafiana na magari barabarani.
- Angalia magari kabla hujafungua mlango. Toka kwenye gari upande wa kizuio ikihitajika.

## 2.25 NI MARUFUKU KUEGESHA

Kuna maeneo mengi ambayo huwezi kuegesha. Angalia alama zinazopiga marufuku au zilizo na vikomo vya kuegesha. Baadhi ya vizuizi vya kuegesha vimebainishwa kwa alama za vizio zilizopo na rangi. **Usiegeshe:**

- Kwenye kivukomilia.
- Mbele ya njia ya umma au ya binafsi.
- Kwenye daraja lolote nje ya vikomo vya jiji au katika barabara kuu.
- Kando ya gari lililosimama au lililoegeshwa (kuegesha maradufu).
- Karibu na futi tano kutoka kwenye bomba la maji ya moto; au katika eneo la alama nyekundu la bomba la maji lililotengwa.
- Karibu na futi 10 kutoka alama ya kusimama.
- Karibu na futi 20 kutoka kiingilio cha kituo cha zimamoto.
- Karibu na futi 50 kutoka kivuko cha reli.
- Katika “MAENEO YA NI MARUFUKU KUEGESHA” ambayo kwa kawaida hutia alama, vizio vya manjano, au alama/mistari ya njia ya miguu.
- Katika mkingamo.
- Kwenye njia ya miguu.
- Kwenye barabara baina ya majimbo na barabara kuu



### KUEGESHA KWA WATU WALIO NA ULEMAVU

Egesha tu katika nafasi iliyotengewa watu walio na ulemavu ikiwa una Kibali cha Kuegesha kwa Watu Walio na Ulemavu. Kwa maelezo kuhusu ustahiki, tembelea [iowadot.gov/mvd/vehicleregistration/Persons-with-disabilities](http://iowadot.gov/mvd/vehicleregistration/Persons-with-disabilities).

## 2.26 KUKARIBIA MAGARI YALIYOSIMAMA SHERIA YA IOWA YA KUENDELEA MBELE AU KUPUNGUZA KASI

Sheria ya Iowa ya Kuendelea Mbele au Kupunguza Kasi inawahitaji madereva wabadilisha vija wakati wanapokaribia gari lolote lililosimama kati ya haya yanayofuata yanayoonyesha taa za kumweka.

- Gari lolote lililosimama kwa ajili ya dharura, kukokotwa, urejesho, ukarabati, ujenzi, uchafu mgumu, au usindikaji taka ambalo limewasha taa zake.
- Gari lolote lililosimama, ikiwa ni pamoja na gari la abiria, ambalo linaendelea kuonyesha taa za hatari.


Ikiwa ubadilishaji kijia hauwezekani, umepigwa marufuku na sheria, au si salama, lazima upunguze kasi na ujitayarisha kusimama. Ingawa hakuna kasi iliyobainishwa, lazima iwe ya kufaa na sahihi kwa hali zilizopo.

**Kukiuka sheria hii kunaweza kusababisha leseni yako kusimamishwa kwa hadi mwaka mmoja.**

## 2.27 ONDOA GARI BARABARANI UNAPOPATA AJALI

Ukihusika katika mgongano bila majeraha, sheria ya Iowa inahitaji kwamba uondoe gari lako kwenye vija vya magari ikiwa gari linaweza kutumika na linaweza kuondolewa kwa njia salama. Kwa kila dakika ambayo kijia cha magari kimezuiwa, hatari ya mgongano wa pili inaongezeka kwa takribani asilimia 2.8. *(Angalia kielelezo cha 2.16)*

Kielelezo cha 2.16: Sheria ya Kuondoa Gari Barabarani



ONDOA MAGARI YALIYOGONGANA KWENYE VIJA  
VYA KUENDESHEA ILI KUSAIDIA KUZUIA MIGONGANO  
MINGINE NA URUHUSU MAGARI YAENDELEE KUKUPITA.

KIJIA CHA DHARURA

**55K**



Kuna takribani  
**migongano 55,000**  
katika jimbo la Iowa  
kila mwaka.



Kila dakika kijia kinapozibwa uwezekano wa  
mgongano mwingine unaongezeka kwa asilimia 2.8.  
**Takribani dakika 30, uwezekano wa mgongano wa  
pili uko juu zaidi.**

**1=4**



Kila **dakika** kijia  
kinapofungwa ni  
sawa na **dakika 4** za  
kuchelewa kwa mabari.



## SURA YA 3

# KUJITAYARISHA KUENDESHA GARI

Kufika unakoenda salama na bila vikwazo kunategemea sana maamuzi na hatua ulizochukua kabla hujawasha gari lako. Hakikisha kuwa wewe na gari lako mko tayari kwa safari ya barabara iliyo mbele.

### 3.1 KUTUNZA GARI LAKO

Kutunza gari lako inavyofaa hakuokoi pesa tu, bali hukupa faida wakati wa dharura. Fuata ratiba ya utunzaji iliyopendekezwa ambayo imeorodheshwa katika mwongozo wa mmiliki wa gari.

#### MFUMO WA BREKI

Magari na malori yanahitaji mifumo miwili tofauti ya breki, breki ya miguu na breki ya kuegesha. Pikipiki na baiskeli moto zinahitaji kuwa na angalau moja. Ikiwa breki zako zinaonekana kuwa na kasoro, zinapiga kelele sana, zina harufu isiyo ya kawaida, au pedali ya breki inaenda kwenye sakafu, mwombe mekanika aziangalie.

## TAA

- Hakikisha kuwa taa, taa za breki, taa za nyuma na taa za mbele zinafanya kazi vizuri kwa kuzikagulia nje ya gari.
- Magari na malori yote yanahitaji taa mbili za mbele ya gari: moja kulia na nyingine kushoto. Pia unahitaji angalau taa moja nyekundu nyuma ya gari, na inapaswa kuonekana kwa angalau umbali wa futi 500. Taa nyeupe ya kumulika kisahani cha nambari ya usajili pia inahitajika.
- Ikiwa gari limewekwa taa za kugeuka, lazima zifanye kazi. Taa za kugeuka zinahitajika kwa magari, malori na matrela yote yaliyo na upana zaidi ya inchi 40.
- Taa ya mbele iliyowekwa vibaya inaweza kuangaza mahali isipokusaidia na huenda ikawazuia madereva wengine kuona. Ikiwa unatatizika kuona usiku, au madereva wengine wanakuwashia taa zao za mbele mara kwa mara, mwombe mekanika aangalie taa za mbele.
- Dumisha usafi wa taa za mbele, nyuma, breki na za nyuma. Uchafu kwenye lenzi unaweza kupunguza ufaafu wa taa kwa asilimia 50.



Kielelezo cha 3.1: Angalia tredi ya gurudumu lako kwa peni

## KIOO CHA MBELE CHA GARI, WAIPA NA SEHEMU ZA JUU ZA KIOO

Chukua hatua zinazofuata ili kuhakikisha kuwa unaweza kuona vizuri unapoendesha gari.

- Badilisha dirisha lolote ambalo limeharibika au limevunika. Kioo kilichoharibika kinaweza kuvunjika kwa urahisi zaidi katika mgongano mdogo au wakati kitu kinagonga kioo cha mbele cha gari. Pia kinaweza kuzuia uwezo wa kuona vizuri.
- Dumisha usafi wa kioo cha mbele cha gari. Mwangaza wa jua au taa za mbele kwenye kioo cha mbele cha gari hufanya kuwa vigumu kuona.
- Hakikisha kuwa kuna maji ya kutosha ya kisafishaji cha kioo cha mbele cha gari na utumie mwosho wa kuzuia kuganda wakati halijoto inaweza kushuka chini ya hali ya kuganda.
- Pangusa theluji, barafu au ukungu kwenye **madirisha yote**. Pangusa madirisha ya mbele, upande na nyuma kabla hujaendesha gari.
- Hakikisha kuwa waipa za kioo cha mbele cha gari, ambazo zinahitajika ziko katika hali nzuri. Ikiwa mabapa ya waipa hayapangusi vizuri kioo cha mbele cha gari, yabadilishe.
- Epuka madirisha yaliyotiwa rangi kupita kiasi. Sheria ya Iowa inahitaji vioo vya mbele vya gari na madirisha kulia au kushoto kwa dereva kuruhusu angalau asilimia 70 ya mwangaza kupita. Iowa haina ondoleo la matibabu kwa madirisha yaliyotiwa rangi. Kwa viwango vya kutia rangi kwenye madirisha nenda kwenye [www.iowadot.gov/mvd/resources/windowtintingstandards.pdf](http://www.iowadot.gov/mvd/resources/windowtintingstandards.pdf).
- Hakikisha kuwa unaweza kuona vizuri. Usitundike vitu kwenye vioo vyako vya nyuma au kujaza vitu kwenye kioo cha mbele cha gari.

## MAGURUDUMU

Magurudumu yaliyoisha au yasiyosawazishwa yanaweza kuongeza umbali wako wa kusimama, kusababisha kuteleza (*Angalia ukurasa wa 60*), kusababisha gurudumu kuisha haraka, kupunguza muda wa fueli na kufanya gari kuwa gumu kudhibiti na kusimama. Gari likidunda, usukani unatingika, au gari linaenda upande mmoja, mwombe mekanika alikague.

- Hakikisha kuwa magurudumu yamejazwa pumzi inavyofaa. Angalia kani hewa ya magurudumu kwa geji ya kani hewa wakati magurudumu ni baridi. **Kani ya gurudumu inayopendekezwa imeorodheshwa kwenye kibandiko ndani ya mlango wa dereva au katika mwongozo wa mmiliki wa gari.**
- Angalia tredi ya gurudumu kwa peni. Weka peni ndani ya tredi “kichwa” kwanza. Tredi isipokuja angalau juu ya kichwa cha Lincoln, gurudumu si salama na linapaswa kubadilishwa. (*Angalia kielelezo cha 3.1*)

## MFUMO WA USUKANI

Ikiwa gari ni gumu kugeuza au haligeuki wakati usukani unageuzwa, mwombe mekanika auangalie usukani.

## MFUMO WA VIANGIKO

Viangiko vyako hukusaidia kudhibiti gari lako na huchochea safari ya starehe kwa sehemu za juu za barabara zinazotofautiana. Gari likidunda sana, au likiendelea kudunda baada ya tuta au baada ya kulisimamisha, huenda ukahitaji shoko mpya au vipande vingine vya viangiko.

## MFUMO WA EKZOSI

Mfumo wa ekzosi husaidia kuondoa gesi mbaya kwenye mtambo, husaidia kupunguza kelele kutoka kwenye mtambo na husaidia kupoza gesi moto inayotoka kwenye mtambo. Moshi kutoka kwenye ekzosi inayovuja unaweza kusababisha kifo kwa muda mfupi sana.

### USIWABI KUACHA MTAMBO WAKO UKINGURUMA

### KWENYE GEREJI, AU KUKAA NDANI YA GARI

### LINALOENDESHA BILA KUFUNGUA DIRISHA.

## MTAMBO

Mtambo usiowekwa vizuri unaweza kupoteza nguvu inayohitajika kwa uendeshaji wa kawaida na dharura, unaweza kukosa kuwaka, hutumia fueli nyingi, huchafua hewa na unaweza kukwama ukiwa barabarani hivyo kusababisha tatizo la msongamano. Fuata taratibu zinazopendekezwa katika mwongozo wa mmiliki wa gari kwa utunzaji.

## HONI

Huenda honi isionekane kama kifaa muhimu cha usalama, lakini kama onyo, inaweza kuokoa maisha yako. Inapaswa kutumiwa tu kama onyo kwa wengine.

## VIOO

Lazima uweze kuona angalau futi 200 nyuma yako katika kioo chako cha nyuma. Ikiwa uwezo wako wa kuona umezuiwa na mzigo, lazima uwe na kioo cha nje. Magari ya vani au aina ya vani lazima yawe na vioo vya nje vya kushoto na kulia.

## 3.2 KUREKEBISHA VITI NA VIOO

Mkao bora wa kiti na kioo ni muhimu ili kudhibiti gari salama. Rekebisha kiti na vioo vya dereva kabla ya kuendesha gari ili kuhakikisha kuwa vimewekwa inavyofaa kwa ajili yako.

### MKAO WA KITI

Kaa huku mgongo wako ukiwa imara kwenye kiti. Kunapaswa kuwa na angalau inchi 10 kati ya usukani na kifua chako, huku mfuko wa hewa ukiashiria kwenye kifua chako.

Sehemu ya juu ya usukani haipaswi kuwa juu zaidi kuliko mabega yako. Sogeza kiti mbele au nyuma ili kisigino chako kiguse sakafu na unaweza kuegemea haraka kati ya breki na kichapuo. Madereva wafuti wanaweza kuhitaji takia la kiti au virefushaji vya pedali ili kukaa salama inchi 10 kutoka kwenye mfuko wa hewa. Kizuizi cha kichwa kinapaswa kuwa katikati ya kichwa cha dereva.

### VIOO

Mbinu iliyo hapa chini inatoa mwonekano bora wa vijia vilivyo kando, kwa usalama wa kutosha.

**Kioo cha ndani:** Kaa wima kwenye kiti cha dereva na urekebishe kioo cha ndani ili kionyeshe dirisha la nyuma lote. Hiki ni kioo kikuu cha kuangalia kile kilicho nyuma ya gari.

**Kioo cha upande wa kushoto:** Egemeza kichwa chako upande wa dirisha la kushoto na uweke kioo cha kushoto ili uone upande wa gari kwa shida. Unapokaa wima, gari halipaswi kuonekana tena katika kioo.

**Kioo cha upande wa kulia:** Egemeza kulia kwa kiweko cha katikati cha gari na uweke kioo cha kulia ili uone upande wa kulia wa gari kwa shida.



### 3.3 MIFUMO MAHIRI YA USAIDIZI KWA DEREVA

Mifumo mahiri ya usaidizi kwa dereva (ADAS) ni vipengele vya teknolojia ambavyo vimeundwa ili kuongeza usalama wa kuendesha gari. Vipengele kama vile breki ya dharura ya kiotomatiki, ufuatiliaji wa sehemu isiyoonekana vizuri na onyo la mgongano wa mbele hutulinda sote, lakini tu ikiwa vinatumika inavyofaa. Ni muhimu kuelewa jinsi vipengele vya ADAS vinavyofanya kazi na vikomo vyake.

Wakati wa mtihani wa udereva, huenda ukasaidiwa na teknolojia za usalama za gari kama vile kamera za nyuma lakini hupaswi kusaidiwa na teknolojia rahisi za gari kama vile kidhibiti cha kasi ya gari.

#### Kielelezo cha 3.2: Teknolojia za magari zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa kwa mtihani

MIFUMO YA KUONYA	INARUHUSIWA KWA JARIBIO
Onyo la nyuma ya gari	Ndiyo
Kifuatiliaji na onyo la sehemu isiyoonekana vizuri	Ndiyo
Teknolojia za kamera (mwonekano wa nyuma, upande, unaozunguka gari)	Ndiyo
Onyo la kasi ya mpindo	Ndiyo
Teknolojia za kugundua (ugunduzi wa baiskeli, anayetembea na vifaa)	Ndiyo
Mifumo ya onyo la mgongano wa mbele	Ndiyo
Tahadhari ya kasi ya juu	Ndiyo
Kifaa cha onyo la kuondoka kwenye kijia	Ndiyo
Sensa za maegesho	Ndiyo
Tahadhari ya magari yanayovuka nyuma	Ndiyo
MIFUMO YA USAIDIZI	INARUHUSIWA KWA JARIBIO
Mifumo ya breki ya dharura ya kiotomatiki au usaidizi wa breki	Ndiyo
Breki ya kurudi nyuma ya kiotomatiki	Ndiyo
Usaidizi wa kusalia kwenye kijia	Ndiyo
Kuepuka mgongano wa kugeuka kushoto	Ndiyo
Udhibiti wa kasi ya gari	Hapana
Kuegesha sambamba kiotomatiki	Hapana

Hata ingawa gari lina vipengele vya teknolojia, lazima uonyeshe uwezo wa kuendesha gari endapo teknolojia zinahitaji dereva kuziondoa kwa mkono, haziwezi kutumika, au dereva anaendesha gari jingine lisilo na teknolojia.

## TEKNOLOJIA ZA MIFUMO YA KUONYA ZA MAGARI

Madhumuni ya msingi ya teknolojia hizi ni kuwapa madereva maonyo katika hali maalum. Teknolojia za mifumo ya kuonya za magari humwarifu dereva kwa onyo, sauti, taa, au mtetemo, kwamba mgongano unakaribia kutokea, au hutoa tahadhari kwamba kuna tatizo au kasoro. Nyingi ya teknolojia hizi ni baridi, kumaanisha zinaonya dereva kuhusu tatizo linaloweza kutokea lakini hazizuii kiotomatiki tatizo au mgongano. Dereva anaweza kufanya mabadiliko kwenye utendaji wa gari ili kuzuia tatizo au mgongano.

### Onyo la nyuma ya gari



**Maelezo:** Hutumia sensa za nyuma kuchunguza vifaa nyuma ya gari na kukutahadharisha ikiwa kifaa kimegunduliwa.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Kipengele cha onyo la nyuma huchunguza nyuma ya gari wakati dereva anabadilisha hadi gia ya kurudi nyuma. Kitakufahamisha – kupitia sauti, mtetemo, au zote – ikiwa kuna kifaa au gari nyuma ya dereva.

Unapaswa kuonyesha tabia zote zinazohitajika ili kufuatilia kwa usalama na kuondoa gari lako unaporudi nyuma. Haya ni pamoja na kuangalia vitu vifuatavyo:

- vioo vya kando
- kioo cha kuona nyuma
- urefu wa mabega (uchunguzi wa kichwa)
- kamera nyingine, ikiwa zimewekwa

### Kifuatiliaji na onyo la sehemu isiyoonekana vizuri



**Maelezo:** Hukuonya kuhusu magari mengine yanayoendeshwa kwenye sehemu zako zisizoonekana vizuri kupitia kuonyesha ishara, sauti, au mtetemo. Onyo la ziada linaweza kutokea ikiwa dereva anatumia taa yake ya kugeuka wakati kuna magari mengine kwenye kijia.

**Jinsi Kinavyofanya Kazi:** Kifuatiliaji cha sehemu isiyoonekana vizuri hukusaidia kufahamu zaidi kuhusu magari mengine. Maonyo yanayotolewa na kifuatiliaji cha sehemu isiyoonekana vizuri yanaweza kusaidia wakati unabadilisha kijia, lakini dereva hapaswi kuridhika mno na kutegemea vifuatiliaji vya sehemu isiyoonekana vizuri pekee kwa ajili ya kubadilisha vijia. Haya ni pamoja na uchunguzi wa mara kwa mara:

- vioo vya kando
- kioo cha kuona nyuma
- urefu wa mabega (uchunguzi wa kichwa)
- kifuatiliaji cha sehemu isiyoonekana vizuri, ikiwa kimewekwa

## TEKNOLOJIA ZA KAMERA

### Kamera ya nyuma



**Maelezo:** Husaidia kuona vitu vilivyo nyuma ya gari moja kwa moja kwa kuonyesha mwonekano mpana nyuma ya gari unoporudi nyuma. Kamera nyingine huonyesha mwonekano mpana kuliko nyingine.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Wakati dereva anabadilisha hadi gia ya kurudi nyuma, kamera ya nyuma inaanza kuonyesha eneo la nyuma ya gari. Kutegemea na gari, skrini ya kuonyesha inaweza kupatikana kwenye kikoa cha katikati, katika kioo cha mwonekano wa nyuma, katika kioo cha punguza mwanga wa jua, au katika maeneo mengine.

Usitegemee tu kamera ya nyuma, endelea kuangalia:

- vioo vya kando
- kioo cha kuona nyuma
- urefu wa mabega (uchunguzi wa kichwa)
- kamera nyingine, ikiwa zimewekwa

### Kamera ya mwonekano wa kando



**Maelezo:** Huonyesha mwonekano mpana wa kijia kando ya gari wakati unatumia taa yako ya kugeuka au unapowasha kipengele hicho mwenyewe. Kipengele hiki kina matumizi sawa na vifuatiliaji vya sehemu zisizoonekana vizuri.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Kipengele hiki hukuonyesha mwonekano wa video wa kile kilicho karibu au kinachokuja kando ya gari lako. Kinaweza kutumika pamoja na, au badala ya vioo vya kawaida. Unaweza kutumia taa ya kugeuka au kuwasha kipengele kupitia kitufe ambacho huwa kwenye wenzu wa taa ya kugeuka. Huenda kipengele hiki kisipatikane unaporudi nyuma au kinaweza kuwaka tu wakati unaendesha gari polepole.

Kamera ya mwonekano wa upande zinapaswa kutumiwa pamoja na vioo vya kawaida na kuangalia urefu wa kichwa (kuangalia kwenye mabega). Magari mengine mapya zaidi yanaweza kuwa na kamera za mwonekano wa upande badala ya vioo vya kawaida.

### Mfumo wa kifuatiliaji cha mwonekano wa mazingira au kifuatiliaji cha mwonekano wa karibu



**Maelezo:** Husaidia madereva kugesha kwa urahisi zaidi kwa kuelewa vizuri mazingira ya gari kupitia mwonekano pepe wa macho ya ndege kutoka juu ya gari. Kifuatiliaji cha mwonekano wa karibu hukusaidia kuthibitisha kwa macho mkao wa gari kuhusiana na mistari iliyo karibu na sehemu za maegesho na vitu vilivyopakana.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Kifuatiliaji cha mwonekano wa karibu huchakata video kutoka kwenye kamera nne, kikionyesha picha mbalimbali kwenye skrini kana kwamba kuna kamera moja ya mwonekano wa macho juu ya gari. Kamera nne za pembe pana mbele, nyuma, kushoto na kulia ni misingi ya kioo cha mwonekano wa karibu.

Kifuatiliaji cha mwonekano wa mazingira au mifumo ya kifuatiliaji cha mwonekano wa karibu inapaswa kutumiwa pamoja na vioo vya kawaida na kuangalia kwenye mabega (ukaguzi wa urefu wa kichwa). Magari mengine mapya zaidi yanaweza kuwa na kifuatiliaji cha mwonekano wa mazingira au mifumo ya kifuatiliaji cha mwonekano wa karibu wa vioo vya kawaida.

## TEKNOLOJIA ZA UGUNDUZI

### Ugunduzi wa baiskeli, anayetembea na vitu



UGUNDUZI WA BAIKELI

**Maelezo:** Hukutahadharisha wakati baiskeli, anayetembea, kitu kinachoenda polepole au kilichosimama kimegunduliwa wakati unaendesha kwa kasi za chini, kwa jumla karibu maili 25 kwa saa. Mifumo mingine inaweza tu kugundua waendeshaji baiskeli, wanaotembea au vitu wanapoenda mbele ya gari na wakati wanaenda upande mmoja. Aina nyingine za ugunduzi wa vitu zitashika breki kiotomatiki.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Sensa zilizo mbele au nyuma (au mbele na nyuma) ya gari zinaweza kugundua jinsi gari lilivyo karibu na baiskeli, anayetembea, au kitu mbele au nyuma. Kwa kawaida hizi zinalingana na rada. Maonyo yanaweza kuwa ya sauti, picha, mitetemo, pigo la breki la haraka, au mchanganyiko wa maonyo. Milio inakuwa ya haraka kadri gari linavyokaribia baiskeli, anayetembea au kitu. Mgongano unakaribia wakati milio inaendelea mfululizo.




UGUNDUZI WA ANAYETEMBEA

Hupaswi kutegemea ugunduzi wa baiskeli, anayetembea wala kitu. Fahamu wakati wote kuhusu mazingira yako na uangalie ikiwa kuna waendeshaji wa baiskeli, wanaotembea, au vitu mara kwa mara, haswa katika maeneo ya mijini.



UGUNDUZI WA KITU



Sensa zinahitaji kusafishwa mara kwa mara ili zifanye kazi inavyofaa.

### Onyo la kasi ya mpindo



**Maelezo:** Hukuonya wakati unakaribia mpindo au njia ya kutoka barabarani haraka sana.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Hufuatilia kasi na eneo la gari kupitia GPS na hukuonya kupunguza kasi unapokaribia mipindo na njia za kutoka.

Hupaswi kutegemea maonyo ya kasi ya mpindo na udumishe kasi salama unapoendesha gari na kukaribia mipindo au njia za kutoka.

## Mifumo ya onyo la mgongano wa mbele



**Maelezo:** Hukutahadharisha kuhusu mgongano unaotarajiwa na gari linaloendeshwa polepole sana au lililosimama au kifaa mbele yako ili ushike breki au upinde ghafla. Onyo pekee halitamshikia dereva breki kiotomatiki. Onyo la mgongano wa mbele huchunguza barabara iliyopo mbele unapoendesha gari.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Sensa zilizo mbele ya gari zinaweza kugundua jinsi gari lilivyo karibu na magari mengine yaliyo mbele yako. Kwa kawaida hizi ni za kamera au za rada. Zimekusudiwa kukuonya wakati unakaribia gari au kitu kilicho mbele. Maonyo yanaweza kuwa ya sauti, picha, mitetemo, pigo la breki la haraka, au mchanganyiko wa maonyo. Mfumo wa onyo la mgongano wa mbele huchunguza magari yaliyo mbele mara 20 kwa sekunde hadi futi 500 mbele ya gari lako na kisha hukuonya kushika breki ikiwa kuna hatari kwenye njia yako. Mfano, hizi hapa ni ngazi tatu za tahadhari\*:

KASI	WAKATI WA ONYO KABLA YA MGONGANO
Maili 15–18 kwa saa	Sekunde 3
Maili 18–50 kwa saa	Sekunde 4
Maili zaidi ya 50 kwa saa	Sekunde 5

Unapaswa kutahadhari wakati wote, angalia magari mara kwa mara na ukae umbali wa kufuata ambao ni salama. Endapo utakaribia gari jingine bila kukusudia, mfumo wa onyo la mgongano wa mbele utakuarifu ili ushike breki au uendeshe gari haraka.

## Tahadhari ya kasi ya juu



**Maelezo:** Husaidia kudumisha kasi salama kwa kutuma tahadhari ikiwa unaendesha gari kwa kasi.

**Jinsi Kinavyofanya Kazi:** GPS au kituo cha habari na burudani cha gari lazima kisasishwe ili kuhakikisha kwamba kasi iliyorekodiwa inajulikana. Ikiwa kasi iliyorekodiwa itapitishwa, tahadhari itawaka kama milio au maonyo ya picha kama vile mabadiliko ya rangi kwenye onyesho au alama ya kikoo cha kasi inayomweka. Onyo likitoa sauti, unapaswa kupunguza kasi kwa makini hadi kikomo cha kasi kilichowekwa kinachofaa kwa kuachilia kichapuo au kushika breki kiasi. Usipige breki kwa nguvu ili kudumisha kasi salama.

Hupaswi kutegemea tahadhari ya kasi ya juu na unapaswa kufuatilia kasi yako mara kwa mara, kudumisha kasi salama na utii kiikomo cha kasi barabarani.

## Kifaa cha onyo la kuondoka kwenye kijia



**Maelezo:** Hukutahadharisha wakati unatoka kwenye kijia chako kwa kutumia maonyo ya picha, mtetemo au sauti. Kipengele hiki kinaweza kukutahadharisha kuendesha gari katikati ya kijia chako ukiondoka kimakosa, kukusaidia kuzuia mgongano.

**Jinsi Kinavyofanya Kazi:** Kipengele hiki kinategemea alama za barabarani ili kufanya kazi. Kimeundwa ili kukutahadharisha gari likianza kutoka kwenye kijia kwa aina moja au zaidi za maonyo.

Usitegemee vifaa vya kuonya vya kuondoka kwenye kijia ili kudumisha mkao sahihi wa kijia.

## Sensa za maegesho



**Maelezo:** Kukutahadharisha mkao wa vitu karibu na gari lako unapoegesha gari.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Gari linaweza kutoa maonyo ya sauti kwamba kuna vitu mbele au nyuma yake. Nafasi baina ya milio zinaweza kuwa fupi zaidi kadri gari linapokaribia kitu. Sauti ya mara kwa mara inamaanisha kuwa gari linakaribia kitu.



Usitegemee tu sensa za kuegesha ili kugundua vitu vyote. Huenda zisigundue vitu ambavyo ni bapa ardhini, chini ya bamba, karibu sana na gari, au mbali sana nalo. Endelea kufahamu mazingira yako kupitia matumizi ya vioo, kukagua urefu wa mabega na kamera za nyuma unapoegesha gari, ikiwa ni pamoja na kufahamu watu au vitu vinavyoweza kuingia katika njia ya maegesho.

## Tahadhari ya magari yanayovuka nyuma



**Maelezo:** Hukuonya ikiwa gari moja au zaidi yanakaribia kuingia kwenye njia ya maegesho. Inaweza kugundua magari yanayoweza kuwa yakivuka wakati unaporudi nyuma.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Sensa karibu na nyuma ya gari hugundua magari mengine yanayokuja kutoka kushoto na kulia. Unaweza kutahadharishwa kwa sauti ya onyo ya taa zinazomweka kwenye vioo au dashibodi ikikuarifu usimame.

Usitegemee tahadhari ya gari linalovuka nyuma na uendelee kufahamu mazingira yako kupitia matumizi ya vioo, kuangalia urefu wa kichwa na kamera za nyuma, ikiwa ni pamoja na kutahadhari watu au vitu vinavyoweza kuingia kwenye njia karibu na sehemu ya nyuma ya gari.

## TEKNOLOJIA ZA USAIDIZI KWA DEREVA

Madhumuni ya msingi ya teknolojia hizi ni kutumia kipengele fulani cha kuendesha gari katika hali mahususi. Teknolojia za mifumo ya usaidizi wa magari huwasaidia madereva kuepuka hatari na migongano. Baadhi hufanya marekebisho kiotomatiki kwenye gari na nyingine husaidia dereva kufanya marekebisho, kama vile kushika breki au kuendesha gari. Bado dereva anaweza kuwa akihitajika kufanya mabadiliko kwenye matumizi ya gari ili kuzuia tatizo au mgongano, lakini gari linasaidia.

## Mifumo ya breki ya dharura ya kiotomatiki au usaidizi wa breki



**Maelezo:** Inaweza kutambua gari linaloendeshwa polepole au lililosimama au kitu kilicho mbele na kushika breki haraka ukishindwa kufanya hivyo.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Ukishindwa kushika breki au kuendesha gari ili kuepuka hatari iliyopo mbele, gari litapunguza kasi haraka au kusimama lenyewe ili kuepuka mgongano. Unapaswa kuendelea kuchunguza hatari kwenye barabara na kudumisha umbali salama wa kufuata gari.



## Breki ya kurudi nyuma ya kiotomatiki



**Maelezo:** Unaweza kushika breki ikiwa kitu kimegunduliwa unaporudisha gari nyuma. Hukusaidia kuepuka mgongano unaowezekana wakati gari linasonga nyuma.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Unaporudi nyuma, ikiwa kitu kimegunduliwa, unaweza kusikia milio ya mfululizo au kuona viashiria vya picha ili kukutahadharisha kwamba kitu kipo nyuma. Usipochukua hatua, breki ya kiotomatiki ya kurudi nyuma inawaka na breki zinashikwa mara moja ili kusaidia kuepuka mgongano unaoweza kutokea.

Usitegemee teknolojia ya breki ya kurudi nyuma ya kiotomatiki. Endelea kuangalia vioo, angalia urefu wa mabega (kagua urefu wa kichwa) na utumie kamera za nyuma ikiwa zimewekwa.

## Usaidizi wa kusalia kwenye kija



**Maelezo:** Kipengele hiki kinaweza kusaidia kukurejesha kwenye kija chako ukiondoka, na kuweza kuzuia mgongano.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Unaweza kupokea tahadhari kupitia sauti, taa inayomweka, au mtetemo ikiwa gari litaondoka kwenye kija chake. Unapaswa kurudi kwenye kija chako; usipochukua hatua, kipengele hiki kinaweza kuendesha gari taratibu hadi kwenye kija chake. Hughairiwa kwa urahisi kwa kudukua gurudumu. Kipengele hiki hakitafanya kazi wakati mistari ya kija ni hafifu ai imefunikwa kwa theluji au uchafu.

Dereva hapaswi kutegemea kisaidizi cha kukaa kwenye kija na anapaswa kuendelea kudhibiti gari wakati wote kwenye barabara na kusalia ndani ya kija cha kuendeshea gari.



## Kuepuka mgongano wa kugeuka kushoto



**Maelezo:** Kipengele hiki hufuatilia magari unapogeuka kushoto kwenye magari kwa kasi ya chini (kama kwenye taa ya barabarani). Huwasha sauti za kuonya na taa za dashibodi na kushika breki kiotomatiki ikiwa unageuka kushoto katika njia iliyo na gari jingine.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Mfumo huu wa kisaidizi cha kugeuka kushoto hufuatilia magari yanayokuja unapoanzisha maneva ya kugeuka kwenye kija cha kuendeshea cha mkabala kwa kasi ya chini. Ikiwa nafasi baina ya magari ni ndogo sana kuruhusu mgeuko, mfumo unazuia gari kusonga mbele.

Mgongano na gari jingine linalokuja ukikaribia, mfumo utasimamisha mgeuko mapema kwa kuanzisha maneva ya breki ya dharura ya kiotomatiki.

Usitegemee mwepuko wa mgongano wa kugeuka kushoto. Unapaswa kuchunguza na kufuatilia kwa usalama mazingira ya kuendeshea gari yaliyo mbele ikiwa kuna hatari na uamue wakati ambao ni salama kugeuka mbele ya gari jingine.

## TEKNOLOJIA RAHISI

Teknolojia zinazofuata zinaleta urahisi kwa dereva na hazihitaji mwombaji kuonyesha ujuzi unaohitajika. Teknolojia rahisi haziruhusiwi kutumiwa wakati wa mchakato wa mtihani wa udereva.

### Udhibiti wa kasi ya gari



**Maelezo:** Zinaweza kuongeza au kupunguza kasi ya gari ili kudumisha umbali unaofuata uliowekwa na dereva. Matoleo ya juu zaidi yanaweza hata kupunguza kasi na kusimamisha gari katika misongamano na kisha kukanyaga mafuta kiotomatiki.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Unakanyaga mafuta kwa kasi uliyoweka na kisha kuwasha kipengele cha udhibiti wa kasi ya gari (ACC). Kisha unaweza kuambia ACC nafasi ya umbali wa kufuata gari jingine unayotaka (kwa jumla mfupi, wastani, au umbali mrefu).


Sensa zilizo kwenye gari zinasoma barabara iliyopo mbele kujua kuhusu magari, kudumisha umbali baina yako na gari lililopo mbele, kupunguza kasi yako ikihitajika ili kudumisha umbali. Hata hivyo, dereva anahitajika kuendelea kufahamu mazingira yake. Katika hali mbaya ya hewa na hali zisizo salama za kuendesha gari, unashauriwa kutotumia kipengele chochote cha kudhibiti kasi ya gari, ikiwemo ACC.

### Kuegesha sambamba kiotomatiki



**Maelezo:** Husaidia kukuongoza kwenye eneo la maegesho sambamba. Bado unawajibikia kushika breki na kufuatilia mazingira.

**Jinsi inavyofanya kazi:** Unaweza kuwasha sensa za kuegesha gari sambamba za kiotomatiki za gari ukiwa tayari kuegesha. Mfumo wa kuegesha gari sambamba wa kiotomatiki utakufahamisha wakati umepata eneo bora la kuegesha. Unapaswa kufuata vidokezo vyovyote vinavyotolewa na gari. Vinaweza kujumuisha kusimamisha gari mbele ya nafasi, kubadilisha hadi gia ya kurudi nyuma na kuondoa mikono kwenye usukani. Dereva anawajibikia kushika breki. Baada ya gari kuegeshwa, unaweza kufanya marekebisho kidogo ili kuhakikisha kuwa gari liko katika mkao bora.



Kagua kwa makini mwongozo wa mmiliki wa gari ili kusoma kuhusu kipengele chochote ambacho ni kipya kwako na uhakikishe kwamba unajua jinsi kinavyofanya kazi. Ikiwa bado una maswali, wasiliana na mwuzaji ili akuelezee.



## 3.4 KUFHAMU MAENEO YASIYOONEKANA VIZURI

Maeneo yasiyoonekana vizuri ni sehemu nje ya gari lako ambazo haziwezi kuonekana kwa kutumia vioo. Maeneo yasiyoonekana vizuri pia yanaweza kusababishwa na viziizi vya kuona kutokana na vifaa vya gari (vioo vya mwonekano wa nyuma, mihimili, nk.) na mazingira yako ya kuendesha gari (miti, jua, nyua, vilima na kuta).

### MAENEO YASIYOONEKANA VIZURI YA MADEREVA WENGINE

(Angalia kielelezo cha 3.3)

- Usiendeshe gari katika eneo lisiloonekana vizuri la dereva mwingine. Ongeza kasi au upunguze kasi ili dereva mwingine aweze kuona gari lako.
- Unapopita gari jingine, toka kwenye eneo lisiloonekana vizuri la dereva mwingine haraka uwezavyo.
- Usiwahi kukaa kando ya gari kubwa kama vile lori au basi. Magari haya yana maeneo makubwa yasiyoonekana vizuri na ni vigumu kwao kukuona.

### MAENEO YAKO YASIYOONEKANA VIZURI

- Fahamu maeneo yasiyoonekana ya kawaida karibu na gari lako yanayoathiri uwezo wako wa kuona nje ya gari lako.
- Tahadhari maeneo yasiyoonekana vizuri unapobadilisha vijia na/au kuingia eneo lenye magari (angalia kielelezo cha 3.3).
- Maeneo yasiyoonekana vizuri yanaweza kuongezeka kutokana na hali za hewa na mwangaza wa mchana. Jua linaweza kuleta maeneo yasiyoonekana vizuri kwa uakisi kwenye sehemu yoyote ya juu ya dirisha lako. Kioo cha mbele ya gari ni sehemu maarufu zaidi ya uakisi na maeneo yasiyoonekana vizuri. Miwani ya jua au matumizi ya vioo vinavyopunguza mwanga katika magari mengi husaidia kukinga macho yako dhidi ya uakisi huo unaofanya kuwa vigumu kuona.

## 3.5 MIKANDA NA VIZUIZI VYA WATOTO


### MIKANDA

Kabla ya kuondoka, kila mtu anapaswa awe amejifunga mkanda inavyofaa. Migongano ya magari ni chanzo nambari moja cha vifo va vijana. Kitu rahisi zaidi unachoweza kufanya kuepuka kuwa miongoni mwa takwimu ni kujifunga mkanda.

Jifunge mkanda wako wa mapajani kwa kubana kwenye nyonga zako. Ikiwa wewe ni mjamzito, unaweza kujifunga vizuri mkanda kwenye fupanyonga, chini ya tumbo lako inapowezekana.

Kutojifunga mkanda kunachukuliwa kuwa kosa la msingi, kumaanisha kwamba unaweza kusimamishwa kwa madhumuni tu ya kutotii sheria ya kujifunga mkanda. Ukiukaji wa sheria hii unaadhibiwa kwa hadi faini ya dola 50 kwa kila abiria na dola 100 kwa kila abiria chini ya umri wa miaka 18.

Kielelezo cha 3.3: maeneo yasiyoonekana vizuri



MIKANDA NI NJIA BORA ZAIDI YA KUZUIA VIFO NA MAJERAHA KWENYE MGONGANO. MBALI NA HILO, UNAVUNJA SHERIA YA IOWA KWA KUTOJIFUNGA MKANDA.

IOWA INAWAHITAJI ABIRIA WOTE WALIOKAA KWENYE VITI VYA MBELE VYA GARI KUJIFUNGA MIKANDA. SHERIA PIA INATUMIKA KWA ABIRIA WANAOKAA KWENYE VITI VYA NYUMA AMBAO WANA UMRI WA CHINI YA MIAKA 18.

## MIKANDA NA SHERIA YA IOWA

- **Mtoto aliye na umri wa chini ya mwaka mmoja na mwenye uzani wa chini ya kilo 20** lazima alindwe katika mfumo wa kizuizi cha mtoto unaoangalia nyuma.
- **Mtoto aliye na umri wa chini ya miaka sita** lazima alindwe katika mfumo wa kizuizi cha mtoto (kiti cha usalama au kiti cha kiongeza nguvu, si mkanda).
- **Mtoto aliye na umri wa chini ya miaka sita hadi 18** must be secured in a child restraint system or by a seat belt, in all seating positions (front and back).
- **Watu wazima walio na umri wa mika 18 na zaidi** lazima wajifunge mkanda wanaposafiria viti vya mbele vya gari.

Vighairi vya matumizi ya mikanda vinaweza kupatikana mtandaoni kwenye:

[iowadot.gov/mvd/medical-exemptions-from-safety-belt-use](http://iowadot.gov/mvd/medical-exemptions-from-safety-belt-use)

## DHANA POTOVU KUHUSU MIKANDA

“Ni chaguo langu kujifunga mkanda na simwathiri yeyote isipokuwa mimi binafsi.”

Ikiwa hujajifunga mkanda inavyofaa wakati wa mgongano, uko kwenye hatari ya kurushwa mbele na kuwajeruhi au kuwaua wengine ndani ya gari. Hata wakati uko peke yako garini, usipofunga mkanda inavyofaa, hali isiyotabirika inaweza kukusababisha upinde au ushike breki ghafla, jambo linalokulazimisha kutoka kwenye kiti cha dereva na kuweza kusababisha mgongano.

“Mikanda ni mizuri kwa safari ndefu, lakini siihitaji ikiwa ninaendesha gari hapa mjini.”

Zaidi ya nusu ya vifo vyote vya magari hutendeka ndani ya maili 25 kutoka nyumbani. Vingi hutokea kwenye barabara zilizo na vikomo vya kasi vya chini ya maili 45 kwa saa.

“Mikanda inaweza kukubania ndani ya gari.”

Huchukua chini ya sekunde moja kufungua mkanda. Dhana hii potovu mara nyingi hurejelea tukio ambapo gari liliwaka moto au kuzama kwenye maji ya kina kirefu. Migongano kama huu hutokea mara chache. Hata kama inatokea, mkanda unaweza kukuzuia kurushwa nje. Uwezekano wako wa kuepuka ajali utakuwa bora ukiwa na fahamu.

“Watu wengine wanatupwa kwenye mgongano na kuenda bila mkwaruzo wowote”

Uwezekano wako wa kutoaga dunia kwenye mgongano ni bora zaidi ukisalia ndani ya gari. Mikanda inaweza kukuzuia kurushwa kutoka kwenye gari lako hadi kwenye njia ya gari jingine.



## 3.6 KUFUNGA VIFAA VILEGEVU

Mbali na kujilinda na kuwalinda abiria wako, unapaswa pia kuhakikisha kuwa hakuna vifaa vilegevu katika gari lako vinavyoweza kumjeruhi mtu endapo utasimama ghafla au kuna mgongano. Kwa maili 55 kwa saa, kifaa cha uzito wa kilo 20 hugonga kwa nguvu zenye uzito wa kilo 1,0000. Pia, hakikisha kuwa hakuna vifaa kwenye sakafu vinavyoweza kuingirira chini ya pedali ya breki na kutatiza kushika breki.

## 3.7 KUONDOA VIVURUGAJI MAWAZO

Kuna aina tatu za vivurugaji mawazo:



**Kuona** – kufanya kitu kinachohitaji dereva kuangalia upande mbali na jukumu la kuendesha gari (mfano, kuangalia kwenye GPS).



**Kutumia mikono** – kufanya kitu kinachohitaji uondoe mkono mmoja au yote miwili kwenye usukani (mfano, kula au kujipaka vipodozi).



**Uzingatifu** – kufanya kitu kinachosababisha akili ya dereva kutanga au kumakinika kwingineko (mfano, kusikiliza muziki au kuzungumza).

Aina zote za vivurugaji zinaweza kuwa hatari wakati unaendesha gari na majukumu mengi ambayo watu hufanya kawaida kwenye usukani yanaweza kufaa katika zaidi ya kategoria moja.

## VIFAA VYA MKONONI NA KUTUMA UJUMBE UNAPOENDESHA GARI

Sheria ya IOWA ya kuendesha gari ukiwa umevurugika mawazo inapiga marufuku matumizi ya simu za mkononi na vifaa vingine vya mawasiliano vya elektroniki vya mkononi kuandika, kutuma, au kuangalia ujumbe wa elektroniki unapoendesha gari. Kabla ya kuandika, kutuma au kusoma ujumbe, barua pepe, au chapisho la mtandao wa kijamii, lazima gari lisimame kabisa nje ya barabara.

Vighairi vya sheria hii ni pamoja na:

- Watumishi wa mashirika ya usalama wa umma wanaotekeleza majukumu yao rasmi.
- Wataalamu wa huduma za afya wanaoshughulikia hali za dharura.
- Mtu anayepokea taarifa inayohusiana na usalama ikiwa ni pamoja na tahadhari za dharura, hali barabarani na hali ya hewa.

## KUZUNGUMZA KWA SIMU

Madereva walio na umri wa chini ya miaka 18 na kibali cha mafunzo, leseni ya wastani au leseni ndogo ya shuleni wanapigwa marufuku kupiga na kupokea simu na kuzungumza kwa simu wanapoendesha gari isipokuwa gari lao liwe limesimama kabisa nje ya barabara.

## UTEKELEZAJI NA ADHABU

Uendeshaji gari ukiwa umevurugwa mawazo unachukuliwa kuwa kosa la “msingi” barabarani—kumaanisha afisa anaweza kukusimamisha kwa ajili ya ukiukaji. Mbali na kulipa faini, mashtaka ya kuendesha gari ukiwa umevurugwa mawazo yanaweza pia kusababisha leseni au kibali chako kusimamishwa au kubatilishwa.

Ukiendesha gari ukiwa umevurugwa mawazo na kusababisha kifo cha mtu mwingine, huenda ukakabiliwa na faini zaidi ya dola 1,000, leseni yako kusimamishwa na kutegemea na hali, kushtakiwa kwa mauaji ya gari.

### 3.8 POMBE NA DAWA ZA KULEVYA

Moja ya sheria zinazotekelezwa zaidi kwenye barabara zote za taifa ni kuendesha gari ukiwa mlevi. Iwa si tofauti, ikiwa na adhabu za juu kwa madereva wanaopatikana wakiwa walevi wa pombe au dawa za kulevya.

#### KUENDESHA GARI UKIWA MLEVI (OWI)

Jina rasmi la kosa la kuendesha gari ukiwa mlevi ni “Kuendesha Gari Huku Ukiwa Umelewa” na hufafanuliwa kama kuwa na pombe kwenye damu (BAC) ya kiwango cha .08 au juu au kuendesha gari ukiwa na kiwango chochote cha mihadarati inayodhibitiwa katika mfumo wako. BAC kwa kawaida hupimwa kupitia kivutapumzi, sampuli ya mkojo au kipimo cha damu. Hata kama hujapatikana na kosa la OWI katika mahakama ya uhalifu, haki zako za kuendesha gari bado zinabatilishwa kwa kiwango cha chini cha siku 180 ukiendesha gari huku ukiwa umelewa. Makosa ya kurudia kwa kuendesha gari huku ukiwa umelewa yanazidi kuwa mabaya, na kusababisha ubatilishaji wa leseni ya dereva kwa muda mrefu na adhabu kali sana za uhalifu.

#### IDHINI YA KUDOKEZA VIPIMO

Ukiwa mmiliki wa leseni ya dereva ya lwa, unakubali idhini ya kipimo cha pombe kwenye eneo kinapohitajika na mamlaka ya utekelezaji sheria (Kanuni ya lwa §321J.6). Sheria hii pia inatumika kwa dereva yeyote asiye mkazi anayesafiri katika jimbo.

#### KUKATAA KUPIMWA

Kukataa kipimo cha kivutapumzi hakuhakikishi kwamba hutapatikana na hatia ya OWI na kukataa kipimo bado kutasababisha ubatilishaji wa leseni yako. Madhara ya kukataa kipimo cha kivutapumzi ni mabaya zaidi kuliko kushindwa kipimo, yakiwa na ubatilishaji wa mwaka mmoja wa leseni yako moja kwa moja na faini ya chini ya dola 1,250.

Ukipatikana na hatia ya kukataa kipimo, mahakama pia yanaweza kuamuru daraja na tathmini ya lazima ya ugonjwa wa matumizi ya mihadarati au kifaa cha kivutapumzi cha binafsi kitasakinishwa kwenye gari lako kwa gharama yako.

#### MADEREVA CHINI YA UMRI WA MIAKA 21

Sheria za kuendesha gari ukiwa mlevi ni kali sana ikiwa uko chini ya umri ambao ni haramu kunywa pombe. Dereva wa umri mdogo anasemekana kuendesha gari akiwa amelewa kwa BAC ya .02 au

zaidi. Haki za kuendesha gari za dereva wa umri mdogo zitabatilishwa kwa muda wa chini wa siku 60 na kwa muda wa chini wa siku 180 ikiwa BAC ni .08 au zaidi. Wakosaji chini ya miaka 18 hawastahiki leseni yenye vikwazo vya muda mfupi huku leseni yao ikiwa imebatilishwa kwa OWI.

#### SHERIA YA CHOMBO WAZI

Ni haramu kusafirisha chombo chotechote cha pombe kikiwa wazi, hakijafunikwa na mtu au abiria yeyote katika gari. Vyombo vilivyo wazi vya vileo vinaweza kusafirishwa kwenye buti la gari. Ukiukaji wa sheria hii unaadhibiwa kama kosa dogo kwa hadi faini ya dola 200 kwa kila dereva na abiria aliye ndani ya gari.

### 3.9 KUENDESHA GARI UKISINZIA

Kuendesha gari ukisinzia ni hatari kama tu kuendesha gari ukiwa mlevi. Madereva wanaosinzia wanahitaji muda mrefu kuchukua hatua, mara nyingi huyumbayumba ndani na nje ya vijia, huondoka barabarani na wana uwezekano zaidi wa kusababisha mgongano. **Unapaswa kupumzika, kuegesha kwenye eneo salama, au kubadilisha madereva** ukitambua jambo lolote kati ya yafuatayo:

- Unaota mchana au mawazo ya kuchanganyikiwa.
- Tatizo la kukumbuka maili chache za mwisho ilizoendesha gari.
- Kuenda miayo mara kwa mara au kusugua macho yako.
- Tatizo la kuweka wima kichwa chako.
- Kutoka kwenye kijia chako, kuendesha gari kwa karibu sana, au kugonga safu za mtetemo.
- Kuhisi kutotulia na kukereka.




**Kuwa macho saa 18 mfululizo kunalemaza kama kuwa na pombe kwenye damu (BAC) ya asilimia 0.08, ambako ni kulewa haramu na hukuweka kwenye hatari sawa kwa mgongano.**

## 3.10 KUJITAYARISHA KWA SAFARI BARABARANI – IOWA 511

Ni vizuri kupanga mapema kabla hujaanza safari yoyote - iwe ni njia ya kawaida au safari ndefu. Endelea kufahamu mambo yanayoweza kuathiri safari yako kama vile hali mbaya ya hewa, ujenzi barabarani, migongano, n.k. Tembelea [www.511ia.org](http://www.511ia.org) au pakua programu ya kifaa cha mkononi ya bila malipo ili upate habari kuhusu hali za usafiri kwa barabara kuu na barabara za jimbo za Iowa.

### Kielelezo cha 3.4: Iowa 511



Pakua programu ya Iowa  
511

[www.511ia.org](http://www.511ia.org)



## SURA YA 4

# UJUZI WA MSINGI WA KUENDESHA GARI

Hakuna mwongozo unaoweza kukufunza kikamilifu jinsi ya kuwa dereva salama. Tafiti zinaonyesha kwamba hatari ya mgongano hupungua kutokana na ujuzi – ujuzi unaoweza kupatikana tu kupitia mafunzo na mazoezi.

### 4.1 KUWASHA GARI

Angalia mwongozo wa mmiliki wa gari kuona taratibu bora za kuwasha gari. Taratibu zinatofautiana kutegemea na ikiwa gari lina utemaji fueli na aina ya gia.

### 4.2 KUBADILISHA GIA

#### GIA YA OTOMATIKI

Unapoendesha gari lililo na gia ya otomatiki, hakuna haja ya kubadilisha gia kwa mkono. Badala yake, kiteuzi cha gia kinawajibikia tu kusogeza gari kwa kutumia safu ya P-R-N-D-L.

**P** – “Park” inafunga gari kwa ajili ya kuegesha

**R** – “Reverse” ya kurudi nyuma

**N** – “Neutral” kuacha mtambo bila kazi

**D** – “Drive” kuendesha gari mbele

**L** – “Low Gear\*\*” kupunguza kasi ya mtambo\*

\*Fahamu: hii pia inaweza kuwakilishwa kama “3, 2, 1” kuonyesha gia ya juu zaidi ambayo gia ya otomatiki inaweza kubadilisha hadi kwao.

## GIA YA MKONO

Kwa magari yanayotumia gia ya kubadilisha kwa mkono, kubadilisha gia kunadhibiti masafa ya kasi ambayo gari linaweza kusafiria. Kutegemea na idadi ya gia zilizopo, lazima dereva aweze kubadilisha kutoka “Neutral” au “1” hadi gia za juu, “2, 3, 4...” ili kuharakisha. Ili kufanya hivi, pedali ya tatu inayoitwa “klachi” hutumiwa kubadilisha kati ya gia.

**Hatua ya 1:** Sukuma chini klachi kwa mguu wako wa kushoto

**Hatua ya 2:** Badilisha kijiti cha gia kwa mkono wako wa kulia

**Hatua ya 3:** Kanyaga polepole pedali ya mafuta huku ukiachilia sawia klachi

Rudia mchakato huu wakati “unabadilisha chini” au wakati unahitaji kupunguza kasi ili kusimama. Mchakato huu pia hutumiwa kurudisha gari nyuma kwa kubadilisha hadi “Reverse” kutoka “Neutral” au gia ya “1”.

## 4.3 KUKANYAGA MAFUTA

Kanyaga mafuta hatua kwa hatua na taratibu. Kujaribu kuwasha gari haraka sana kunaweza kusababisha magurudumu kuzunguka, haswa kwenye sehemu telezi, na kusababisha gari kuteleza. Kwa gari la kubadilisha kwa mkono, jifunze kutumia klachi na kichapuzi ili mtambo usiende kwa kasi wala kukwama unapobadilisha gia.

## 4.4 KUFUNGA BREKI NA KUSIMAMISHA GARI

Kutumia breki za gari lako ili kusimama ni moja ya ujuzi muhimu zaidi wa kujifunza. Muda ambao unachukua magurudumu yako kusimama unategemea uzito, ukubwa na kiwango cha kazi na pia hali ya magurudumu yake. Muda wa kuchukua hatua kuweka mguu wako kwenye pedali ya breki pia ni muhimu. Kujifunza jinsi ya kusimamisha gari taratibu na kwa ufanisi kunaweza kuhitaji mazoezi.

Hata ikiwa gari lako na matendohiari yako, sehemu za juu za bado kutaathiri unavyosimamisha haraka. Barabara za changarawe legevu, theluji na barafu au hata njia ya miguu kavu inaweza kusababisha gari lako kuteleza ikiwa breki zitafungwa kwa nguvu sana. Kasi za juu, linachukua muda mrefu kusimama. (*Angalia kielelezo cha 4.1*)

### Kielelezo cha 4.1: Umbali wa kusimama

## UMBALI WA KUSIMAMA

UMBALI WA HATUA YA HATARI + UMBALI WA KUFUNGA BREKI = UMBALI WA KUSIMAMA

maili  
kwa saa

$$20 \text{ Futi } 44 + \text{ Futi } 25 = \text{ Futi } 69$$

$$30 \text{ Futi } 66 + \text{ Futi } 57 = \text{ Futi } 123$$


$$40 \text{ Futi } 88 + \text{ Futi } 101 = \text{ Futi } 189$$

$$50 \text{ Futi } 110 + \text{ Futi } 158 = \text{ Futi } 268$$

$$60 \text{ Futi } 132 + \text{ Futi } 227 = \text{ Futi } 359$$

$$70 \text{ Futi } 154 + \text{ Futi } 310 = \text{ Futi } 464$$

## Kielelezo cha 4.2: Sheria ya sekunde 3 hadi 4



Angalia gari lililo mbele yako likipita mnara, kama vile alama na uanze kuhesabu polepole. Ili kufanikisha umbali salama kufuata gari jingine, bamba lako la mbele halipaswi kupita mnara kabla hujahesabu hadi tatu.

## UMBALI SALAMA WA KUFUATA GARI JINGINE

Kwa kuwa uwezekano mkubwa zaidi wa mgongano uko mbele yako, kutumia sheria ya sekunde 3 hadi 4 kutakusaidia kupata na kudumisha umbali salama wa kufuata gari jingine na kutoa muda wa kutosha kwako kufunga breki ili kusimama ikihitajika. Sheria hii inafanya kazi tu katika barabara ya kawaida ya hali nzuri za hewa. (Angalia kielelezo cha 4.2)

- Dereva asiye na ujuzi au anayeanza kuendesha gari anapaswa kudumisha angalau umbali wa kufuata gari jingine wa sekunde tatu katika hali za kuendesha gari za kawaida.
- Umbali wa kufuata gari jingine wa sekunde mbili unaweza kutosha katika hali za kawaida kwa dereva mwenye ujuzi.
- Kwa kasi za maili 40 kwa saa, umbali wa kufuata gari jingine wa sekunde tano unapendekezwa. Wakati hali za barabarani ni telezi au gari lililo mbele yako linazuia uwezo wako wa kuona, umbali wa kufuata gari hilo wa sekunde sita au zaidi unapendekezwa.

## ABS (MFUMO WA KUZUIA MAGURUDUMU KUJIFUNGA UNAPOFUNGA BREKI)

Magari mengi mapya zaidi yana ABS (mfumo wa kuzuia magurudumu kujifunga unapofunga breki). Hakikisha kuwa umesoma mwongozo wa mmiliki wa gari kuhusu jinsi ya kutumia ABS. ABS itakuruhusu kusimamisha gari bila kuteleza. Ikiwa gari lako lina ABS na unahitaji kusimama haraka:

- Bonyeza pedali ya breki kwa nguvu kadri uwezavyo na uendelee kubonyeza.
- Huenda ukahisi pedali ya breki ikisukuma nyuma wakati ABS inafanya kazi. Usiachilie pedali ya breki. ABS itafanya kazi tu pedali ya breki ikisukumwa chini.

## KUTUMIA TAA ZA BREKI KUWASILIANA NA MADEREVA WENGINE

Ikiwa unataka kusimama au kupunguza kasi kwenye sehemu ambapo dereva mwingine hatarajii, au ikiwa gari lililo nyuma yako linafuata kwa karibu sana, gusa pedali ya breki yako mara tatu au nne haraka. Hatua hii itamfahamisha aliye nyuma yako kuwa unakaribia kupunguza kasi.

## UNAPOHITAJIKA KUSIMAMA

**Lazima usimame wakati wote:**

- Kwenye alama zote za kusimama.
- Kabla ya kuvuka njia ya miguu unapotoka kwenye njia ya binafsi, kichocho, n.k.
- Unapoingia kwenye barabara ya umma kutoka njia ya binafsi, lakini si tu, maegesho, biashara, shule, vituo vya mafuta.
- Kwa ombi la afisa yeyote wa sheria.
- Unapoagizwa na mdhibiti wa magari kwenye eneo la kazi ya ujenzi.
- Kwenye taa nyekundu inayomweka, kisha uende ikiwa barabara haina magari.
- Kwenye taa nyekundu za barabarani, ikiwa ni pamoja na mahali migeuko ya kulia kwenye taa nyekundu inaruhusiwa.
- Wakati mtu aliye na matatizo ya kuona na fimbo (mara nyingi huwa na ncha nyeupe au nyekundu) au mbwa wa kuongoza anatembea mbele yako au karibu na wewe, mtu huyo anaweza kuwa kwenye hatari.

Angalia ukurasa wa 11 kuhusu kusimama kwenye vivuko vya reli na ukurasa wa 19 kuhusu kusimama wakati unapokaribia mabasi ya shule yanayowasha taa na/au mikono ya kusimama.



## 4.5 KASI INAYOFAA

Kikomo cha kasi kilichowekwa ni kasi ya JUU ZAIDI unayoweza kuendesha gari kisheria **kulingana na hali zinazofaa za kuendesha gari**. Kasi yako inapaswa kutegemea kikomo cha kasi kilichowekwa, hali za barabara na hali ya hewa. Kadri gari linavyoendesha kwa kasi, ndivyo umbali zaidi utakaochukua kugeuka, kupunguza kasi au kusimama. Kwa mfano, gari linaloendesha maili 60 kwa saa litasafiri mara 3 mbali zaidi kuliko gari linaloendesha maili 30 kwa saa kabla ya kusimama. (*Angalia kielelezo cha 4.1*)

**Endapo hakuna kikomo cha kasi kilichowekwa, vikomo vinavyofuata vya jumla vimewekwa:**

- Maili 25 kwa saa katika wilaya yoyote ya biashara
- Maili 25 kwa saa katika wilaya ya makazi au wilaya ya shule
- Maili 45 kwa saa katika wilaya yoyote ya kiungani
- Maili 45 kwa saa kwa gari lolote linalokokota gair jingine
- Maili 50 kwa saa kwenye barabara mbadala zisizo na lami kutoka machweo hadi macheo na kwa malori yote kwenye barabara mbadala wakati wowote mchana
- Maili 55 kwa saa kwenye barabara zote za msingi, barabara kuu za mji na barabara mbadala, ikiwa ni pamoja na barabara zisizo za lami kuanzia macheo hadi machweo
- Maili 70 kwa saa kwenye barabara kuu za jimbo vijijini

Kikomo cha chini kinaweza kuwekwa kwa hali yoyote iliyoorodheshwa hapo juu.

Ingawa kuendesha gari kwa kasi zaidi ni chanjo kikuu cha migongano, kuendesha gari polepole zaidi pia kunaweza kusababisha mgongano. Jaribu kuendesha gari kulingana na mtiririko wa magari wa jumla kwenye barabara yoyote. Kwenye mfumo wa barabara kuu za majimbo kuna kasi ya chini ya maili 40 kwa saa. Magari ambayo hayawezi kuenda kwa kasi kulingana na hali za kawaida hayaruhusiwi kwenye barabara kuu za majimbo.

## 4.6 KUZUNGUSHA USUKANI

### KUSHIKA GURUDUMU

Ili kupunguza hatari ya majeraha kutokana na mifuko ya hewa ya mbele na kudhibiti vyema gari lako, tumia klachi inayofaa. Mikono yako inapaswa kuwekwa pande mkabala za usukani saa 9 na 3 au chini kidogo saa 7 na 5. (*Angalia Kielelezo cha 4.3*)

- Angalia vizuri barabarani, si tu sehemu ya mbele iliyopo ulipo. Angalia hali za barabarani pale unapohitaji kuendesha gari kabla hujazifikia. Kwa kufanya hivi, una muda wa kuendesha gari taratibu na kwa usalama.
- Unapokata kona, geuza usukani kwa kutumia mbinu ya “hand-over-hand” au “push-pull”.
- Usigeuze gurudumu kwa kiganja cha mkono mmoja; huenda ukashindwa kudhibiti. Unapokamilisha mgeuko, nyosha usukani kwa mkono. Kuuacha kuteleza kwenye vidole vyako kunaweza kuwa hatari.

Kielelezo cha 4.3: Mkao wa mkono kwenye usukani



## 4.7 KURUDI NYUMA

Ni vigumu kudumisha udhibiti unaporudisha gari nyuma. Kurudi nyuma kunapaswa kufanywa kwa kasi ya polepole. Tumia kichapuzi kwa makini, ikihitajika.

- Kurudi nyuma kunahitaji ugeuze kichwa chako ili uone mbali na kizuizi cha kichwa. Usitegemee vioo wala kamera za nyuma pekee kwa kuwa hazitoi mwonekano kamili na huenda vikapotosha katika dhana ya ndani.
- Badilisha nyonga zako na ugeuke ili uone vizuri nyuma ya gari. Weka mkono wako wa kulia juu ya nyuma ya kiti, shika juu ya usukani kwa mkono wako wa kushoto na uangalie juu ya bega lako la kulia kupitia dirisha la nyuma.
- Angalia maeneo yote ya nyuma ya gari na maeneo yasiyoonekana vizuri ya gari kabla ya na unaporudi nyuma.
- Achilia breki, kisha tumia kichapuzi taratibu na inapohitajika tu, kudhibiti kasi. Endesha poleple.
- Geuza gurudumu lako upande unaotaka gari liende.
- Angalia upande ambao gari linaenda kupitia madirisha ya upande wa nyuma.

## 4.8 MBINU BORA ZA KUGEUZA GARI

Panga migeuko yako mapema. Amua mahali unapotaka kuwa unapokamilisha migeuko. Jipe nafasi ya kupunguza kasi na kuangalia wanaotembea na magari mengine. Migeuko mikali ya dakika za mwisho ni hatari na inapaswa kuepukwa.

Usikate kona na usiende upande sana kwenye migeuko yako. Vitendo hivi vinaongeza uwezekano wa kusababisha mgongano.

## TAA ZA MGEUKO

Taa za mgeuko zinawaambia wengine unachotaka kufanya na kuwapa muda wa kuchukua hatua. Unapaswa kutumia taa za mgeuko kabla hujabadilisha vijia, kugeuka kulia au kushoto, kuingia kwenye barabara, au kuegesha.

- Ashiria kwa taa kila wakati unapobadilisha upande unaoenda. Ashiria kwa taa hata wakati huoni mtu mwingine yeyote karibu. Huenda kukawa na magari, wanaotembea, au waendeshaji baiskeli katika eneo usiloona vizuri. Ni rahisi kukosa kumwona mtu anayehitaji kujua kile unachofanya.
- Sheria ya lowa inakuhitaji uashirie kwa taa angalau futi 100 kabla ya mgeuko ikiwa kikomo cha kasi ni maili 45 kwa saa au chini na ikiwa kikomo cha kasi ni cha haraka kuliko maili 45 kwa saa, lazima uashirie kwa taa angalau futi 300 kabla hujageuka.
- Kama desturi, ashiria kwa taa kabla hujapunguza kasi.
- Kuwa makini ili usiashirie kwa taa mapema sana. Ikiwa kuna barabara, njia za binafsi, au njia za kuingia kati yako na mahali unapotaka kugeuka, subiri hadi uzipite ili uashirie kwa taa.
- Ikiwa gari jingine linakaribia kuingia barabara kati yako na unapotaka kugeuka, subiri hadi ulipite ili uashirie kwa taa mgeuko wako. Ukiashirie kwa taa mapema, dereva mwingine anaweza kudhani kwamba unapanga kugeuka mahali ambapo dereva huyo yupo na huenda akasimama kwenye njia yako.
- Hakikisha kwamba taa ya mgeuko imezimwa baada ya kugeuka.

## MIGEUKO KWENYE TAA NYEKUNDU, BAADA YA KUSIMAMA

Kwenye taa ya barabarani, unaweza kugeuka kulia kwenye taa nyekundu isipokuwa kuwe na alama ya “NI MARUFUKU KUGEUKA KWENYE TAA NYEKUNDU”. Kabla ya kugeuka salama, lazima usimame kabisa na uachie njia magari mengine yote na wanaotembea.

Pia unaweza kugeuka kushoto kwenye taa nyekundu ikiwa unageuka kutoka kijia cha kushoto cha barabara ya upande mmoja kuingia kwenye barabara nyingine ya upande mmoja.

## MANEVA ZA KUGEUKA

### Migeuko ya U

Migeuko ya U inapaswa tu kufanywa mahali ambapo matumizi yake si marufuku na ni salama kufanya hivyo.

### Migeuko ya mara tatu

Migeuko ya mara tatu kwa jumla si maneva salama na inaweza kuongeza hatari na kukusababishia migongano. Ni vizuri kuendelea kuendesha gari hadi mkingamo wa karibu.


## 4.9 KUBADILISHA VIJIA

Mabadiliko ya vijia ni pamoja na:

- Kubadilisha kutoka kijia kimoja hadi kingine.
- Kuingia kwenye barabara kutoka njia ya kuingia.
- Kuingia kwenye barabara kutoka kwenye viziwi au kijia cha dharura.

Badilisha vijia tu kimoja kwa wakati mmoja. Kabla ya kubadilisha vijia, angalia magari karibu nawe na uthibitisha kuwa kuna nafasi ya kuingia salama kwenye kijia na uachie njia gari lolote ambalo tayari liko katika kijia hicho (*angalia kielelezo cha 4.4*).

Kielelezo cha 4. 4: Kubadilisha vijia



**Ashiria kwa Taa:** Wafahamishe madereva wengine kuhusu mipango yako kwa kuashiria kwa taa inavyofaa.



**Dumisha kasi:** Unapobadilisha kijia chako, fanya kwa uangalifu lakini bila kupunguza kasi isipokuwa uwe unaingia katika kijia kilicho na magari yanayoenda polepole. Unapobadilisha vijia, angalia mara kwa mara magari ili uone yeyote anayekuja ulipo bila kutarajia.



**Angalia vioo vyako:** Angalia katika mwonekano wako wa nyuma na vioo vya pembeni. Hakikisha kuwa hakuna magari kwenye kijia unachotaka kuingia. Hakikisha kuwa hakuna mtu anayetaka kukupita.



**Angalia maeneo yako yasiyoonekana vizuri:** Angalia juu ya bega lako upande unaopanga kuenda. Hakikisha kuwa hakuna mtu karibu na kona za nyuma za gari lako.

Unapogeuzi kichwa chako kuangalia maeneo yasiyoonekana vizuri, hakikisha kuwa umenyosha usukani; watu wana hulka ya kawaida ya kugeuzi mikono yao upande sawa na kichwa chao.



**Angalia watumiaji wengine wa barabara:** Hakikisha kuwa umeangalia kijia cha mbali, ikiwa kipo, kwa kuwa huenda mtu katika kijia hicho anapanga kusonga kwenye kijia sawa na unachotaka kuingia.

## 4.10 KUPITA GARI

Pita gari jingine tu wakati alama (ukurasa wa 8) au ishara za barabarani zinakuruhusu kupita (kielelezo cha 4.5), NA umetambua kwamba una nafasi ya kutosha ya kupita salama. Pita tu wakati inahitajika.


- Kama kanuni, pita tu gari moja kwa wakati.
- Epuka kupita katika sehemu ambapo gari linaweza kuingia kwenye barabara mbele yako kama vile mikingamo na njia za binafsi.

Ikiwa kupita kunahitajika, fuata hatua zilizo hapa chini:

1. Angalia kijia cha kupita kilicho mbele ili kuhakikisha kuwa kuna nafasi ya kutosha kabla hujajaribu kupita.
2. Angalia vioo na maeneo yasiyoonekana vizuri kuona magari.
3. Ashiria kwa taa nia ya kupita na uendeshe kwa kasi inayohitajika.
4. Unapopita, fuatilia nafasi iliyo mbele na nyuma ya gari lako na uangalie kioo cha mwonekano wa nyuma.
5. Unapoona mbele ya gari ulilopita katika kioo cha mwonekano wa nyuma na gari lako linaonekana vizuri, ashiria kwa taa nia, rudi taratibu na polepole kwenye kijia cha awali, ghairi taa na urudi kwenye kasi salama.


## ALAMA ZA NJIA YA MIGUU ZINAONYESHA SHERIA ZA KUPITA

Kielelezo cha 4.5: Alama za njia ya miguu zinazoonyesha sheria za kupita




**MSTARI WA KATIKATI WA MANJANO MARADUFU WENYE MISTARI MIEUPE YA KIJIA ILIYOKATIKAKATIKA**

Hakuna kupita njia yoyote kwenye mistari ya manjano ya katikati. Mistari mieupe iliyokatikakatika inatenganisha magari yanayoenda upande mmoja. Kupita kunaruhusiwa wakati mistari mweupe uliokatikakatika uko katika kijia chako.



**MISTARI YA MANJANO THABITI NA ILIYOKATIKAKATIKA**

Usipite wakati mistari thabiti uko katika kijia chako. Katika mfano huu, kijia cha kushoto hakiwezi kupita. Magari kwenye kijia cha kulia yanaweza kupita.




**MSTARI WA KATIKATI WA MANJANO MARADUFU**

Hakuna kupita katika kijia chochote.


- Mistari ya manjano inatenganisha magari yanayoenda pande tofauti
- Mistari mieupe inatenganisha magari yanayoenda pande moja

## KUPITA NI HARAMU KATIKA HALI ZIFUATAZO:

### Kielelezo cha 4.6: Hali haramu za kupita




Usipite wakati unakaribia juu ya kilima.



Usipite wakati unaenda karibu na mpindo mwonekano wako kando ya barabara unapozuiwa.




Usipite ndani ya futi 100 za daraja jembamba, daraja refu, au njia ya chini kwa chini iliyowekwa alama kukufahamisha kuwa ipo.



Usipite ndani ya futi 100 za kivuko cha reli.



Usipite ndani ya futi 100 za mkingamo.



Usipite kulia.



Usivuke wakati gari linalokuja liko karibu sana hivi kwamba inaweza kuwa hatari kujaribu kufika karibu na gari analopita.

## 4.11 KUENDESHA GARI KWA KUPUNGUZA HATARI

Unapoendesha gari salama na kutumia mbinu za kuendesha gari kwa kupunguza hatari, unafahamu na kuwa tayari kwa chochote kitakachotokea. **Asilimia 94 ya migongano mibaya inatokana na machaguo hatari na makosa ambayo watu hufanya wakiwa usukani.** Fuata mbinu hizi za kuendesha gari kwa kupunguza hatari ya kuhusika katika mgongano:

### 1. Fikiria usalama kwanza.

Kuepuka tabia za kuendesha gari kwa fujo na kutomakinika mwenyewe kutakuweka katika nafasi nzuri ya kukabiliana na machaguo ya watu wengine ya kuendesha gari. Acha nafasi ya kutosha kati yako na gari lililo mbele yako. Jifunge mkanda wako kila wakati ili kujikinga dhidi ya kutupwa kutoka kwenye gari katika mgongano.

### 2. Fahamu mazingira yako – makinika.

Angalia voo vyako mara kwa mara na uchunguze hali sekunde 20 hadi 30 mbele yako. Zungusha macho yako mara kwa mara. Ikiwa dereva mwingine anaonyesha dalili za kuendesha gari kwa fujo, punguza kasi au simama kando ili kumwepuka. Ikiwa dereva anaendesha gari kwa njia ya hatari hivi kwamba una wasiwasi, jaribu kuondoka barabarani kwa kugeuka kulia au kuondoka kwa njia ya kutoka inayofuata ikiwa ni salama kufanya hivyo. Pia, tupia macho wanaotembea, waendeshaji baiskeli na wanyama barabarani.

### 3. Usitegemee madereva wengine.

Wafikirie wengine lakini jijali kwanza. Usidhani kwamba dereva mwingine ataondoka barabarani au kukuruhusu uingie. Chukulia kwamba madereva wataendesha magari kupita taa nyekundu au alama za kusimama na ujitayarisha kuchukua hatua. Panga miondoko yako ukitarajia hali mbaya.

### 4. Fuata sheria ya sekunde 3 hadi 4. (Angalia kielelezo cha 4.2 kwenye ukurasa wa 40)

Dumisha umbali salama wa kufuata gari jingine ili kuruhusu muda wa kuchukua hatua ikihitajika.

### 5. Dumisha kasi ya chini.

Vikomo vya kasi vilivyowekwa vinatumika kwenye hali bora. Ni jukumu lako kuhakikisha kuwa kasi yako inalingana na hali. Vilevile, kasi za juu hufanya kuwa vigumu sana kulidhibit gari lako wakati kuna tatizo.

### 6. Kuwa na njia mbadala.

Katika hali zote za kuendesha gari, njia bora ya kuepuka hatari zinazoweza kutokea ni kuweka gari lako mahali ulipo na uwezekano bora wa kuona na kuonwa. Kuwa na njia mbadala ya kusafiri pia ni muhimu, hivyo jitengee kila wakati mahali pa kusogeza gari lako ikiwa njia yako ya karibu itafungwa ghafla.

### 7. Ondoa vivurugaji mawazo.

Uvurugaji mawazo ni shughuli yoyote inayoondoa makini yako kwenye jukumu la kuendesha gari. Kuendesha gari kunahitaji makini yako yote ili uendelee kumakinikia jukumu la kuendesha gari.

## 4.12 KUENDESHA GARI SALAMA KWENYE MSONGAMANO

### ENDESHA GARI KULINGANA NA MSONGAMANO

Magari yanayosonga haraka au polepole kuliko mtiririko wa magari barabarani husababisha ongezeko la idadi ya mabadiliko kwenye vijia, kupita na matukio ya kufuata magari mengine kwa karibu sana. Hali hii huongeza uwezekano wa migongano kati ya magari. Barabara salama zaidi ni wakati magari yote yanasafiri kwa kasi sawa lakini hayazidi kikomo cha kasi.

### MAGARI YANAYOSONGA POLEPOLE

Kuwa tayari wakati wote kubadilisha kasi yako ili ilingane na kasi ya magari barabarani. Magari mengine hayawezi kusafiri haraka au yanatatizika kudumisha mtiririko wa magari barabarani. Ukiyaona magari haya mapema, una muda wa kubadilisha vijia au kupunguza kasi kwa njia salama. Kupunguza kasi ghafla kunaweza kusababisha mgongano.

Magari ya shambani, magari yanayokokotwa na farasi na magari ya kukarabati barabara kwa kawaida husafiri kwa kasi za chini. Magari haya yanaweza kuwa na alama ya magari yanayosonga polepole (pembetatu ya chungwa au taa zinazomweka) kwenye mgongo.

### KUFUATA GARI JINGINE

Migongano mingi inasababishwa na kufuata gari lililo mbele yako kwa karibu sana. Lazima uweze kusimama kabla hujagonga chochote kilicho mbele yako. Kasi za juu zinahitaji usimame kwa umbali mkubwa. Kumbuka hili unapofuata gari jingine. Njia salama na rahisi zaidi ya kujua umbali salama wa kufuata ni kutumia “Three-Four Second Rule” (*angalia kielelezo cha 4.2 kwenye ukurasa wa 40*). Hatua hii itaweka magari yaliyo mbele yako umbali wa kutosha ili kuweza kusimama salama ikihitajika.

### KUENDESHA GARI KWA KARIBU SANA

Ikiwa mtuu anaendesha gari karibu nawe sana, songa kidogo kulia na umpe mfuataji wa karibu mwonekano bora wa kile kilicho mbele na uashirie kwa taa mapema kwa ajili ya migeuko, kusimama au kubadilisha vijia. Jaribu kupunguza kasi na kumhimiza dereva aliye nyuma yako apite. Endapo hilo halitafaulu, ondoka kwenye barabara.



## 4.13 KUWASILIANA - TAA ZA MBELE, HONI NA TAA ZA DHARURA

Madereva wengine hawatilii maanani kile kinachoendelea karibu nao. Migongano mara nyingi hutokea kwa sababu dereva mmoja haoni dereva mwingine, au wakati dereva mmoja anafanya kitu ambacho dereva mwingine hakitarajii. Ni muhimu kwa madereva kuwajulisha watumiaji wengine wa barabara kwamba wapo, na kile wanachopanga kufanya.

### TAA ZA MBELE

Mbali na kukusaidia kuona usiku, taa za mbele huwasaidia madereva wengine kukuona. Washa taa zako za mbele kila unapotatizika kuona magari mengine, kwa kuwa huenda wanatatizika kukuona. Mifano ni pamoja na ukungu, mvuo kubwa, au theluji.

Magari mengi yana taa za mbele zinazowaka kiotomatiki, lakini katika hali nyingine, kama vile dhoruba za theluji mchana, taa ya pande zote ina mwangaza wa kutosha kwa hivyo taa za mbele zinapaswa kuwashwa kwa mkono.

Sheria ya lowa inahitaji matumizi ya taa za mbele kuanzia machweo hadi macheo au wakati mwonekano ni futi 500 au kidogo, (ukungu, mvua kubwa, theluji, nk.). Sheria nzuri ya kidole gumba ni kuwasha taa za mbele kila unapowasha waipa zako.

### HONI

Katik hali fulani, honi yako inaweza kutumika kupata makini ya dereva mwingine na kuzuia mgongano. Tumia honi yako wakati:

- Anayetembea au waendeshaji basikeli wanaonekana kusonga katika kijia chako.
- Unampita dereva anayeanza kuingia kaitka kijia chako.
- Kuna dereva ambaye hamakiniki au huenda anatatizika kukuona.
- Unakuja sehemu ambapo huwezi kuona kilicho mbele, kama vile kichocho chembamba cha kutoka.
- Gari jingine liko katika hatari ya kukugonga.
- Unahitaji kutahadharisha magari mengine, madereva wengine, wanaotembea, au wanyama kuhusu uwepo wako.
- Umeshindwa kudhibiti gari lako na unaenda upande ambao mtu yupo.

### TAA ZA MBELE

Ikiwa gari lako litaharibikia barabarani, hakikisha kwamba madereva wengine wanaweza kuliona. Mara nyingi migongano hutokea kwa sababu dereva hakuona gari ilililokwama na hivyo kuchelewa kusimama. Hii hapa baadhi ya miongozo ikiwa una tatizo la gari na lazima usimame.

- Ikiwezekana, ondoa salama gari lako barabarani na mbali na magari.
- Washa taa za dharura ili kuonyesha kwamba una tatizo.
- Ikiwa huwezi kuliondoa gari lako barabarani, jaribu kusimama mahali ambapo madereva wengine wanaweza kuona vizuri gari lako. Usisimame tu juu ya kilima au karibu tu na mpindo.
- Ikiwa umekwama ndani ya kijia cha magari, wewe na abiria wako mnapaswa kuliondoa gari haraka na kusimama katika eneo salama; inapowezekana, mbali na kijia cha dharura cha barabarani na mbali na magari yanayoendeshwa.
- Fahamisha mamlaka husika kwamba gari lako au la mtu mwingine limeharibika.



*Ukurasa huu umeachwa mtupu makusudi.*



## SURA YA 5

# KUTUMIA UJUZI WAKO KUENDESHA GARI

---

Kwa kuwa sasa tumeangazia mambo mengi ya msingi, sasa ni wakati wa kujifunza jinsi maarifa yako ya kuendesha gari yanatumika kwenye matukio na mazingira tofauti. Vilevile, pia utajifunza mbinu za kuendesha gari katika hali usizotarajia, kama vile hali mbaya ya hewa na dharura.

### 5.1 MIKINGAMO


Mikingamo ni sehemu yoyote ambapo magari yanaungana na mengine au yanavuka. Inajumuisha: barabara za kuvuka, barabara za kando, njia za binafsi, maegesho na barabara za usafiri wa umma.

**Hatua ya 1:** Kabla hujalingia kwenye mkingamo, angalia mbele ili utambue aina ya mkingamo na vifaa vyovyote vya kudhibiti magari (alama, taa za barabarani na alama za njia ya miguu).

**Hatua ya 2:** Chunguza mkingamo kabla hujaeendelea kuhakikisha kwamba njia haina chochote kupitia kwenye mkingamo.

**Hatua ya 3:** Angalia kushoto, kulia na kushoto tena kwa magari yanayokuja na wanaotembea. Usiwahi kuchukulia kwamba dereva mwingine atashiriki nafasi nawe au kukupa nafasi.

Fahamu taa ya mgeuko wa “uongo”. Usigeuke tu kwa sababu gari linalokuja limewasha taa ya kugeuka. Dereva anaweza kupanga kugeuka zaidi yako au amesahau kuzima taa za ishara kutoka mgeuko wa awali. Huu ni ukweli haswa pikipiki; taa zao mara nyingi hazizimiki zenyewe. Subiri hadi dereva mwingine aanze kugeuka kisha kuendelea ikiwa ni salama kufanya hivyo.



Kielelezo cha 5.1: Kuvuka au kugeuka kushoto kwenye barabara ya kijijini ya vijia vinne

## KUVUKA AU KUGEUKA KUSHOTO KWENYE BARABARA YA KIJIJINI YENYE VIJIA VINNE

(Angalia kielelezo cha 5.1) Usijaribu kuvuka pande zote mbili za magari kwa wakati sawa ili kuepuka kusimama wastani. Vuka salama mkingamo huu kwa kufuata hatua zinazofuata:

1. Simama kwenye alama ya kusimama, angalia kushoto na uendeleo kwenye wastani wakati ni salama kufanya hivyo.
2. Endelea kusimama katika wastani. Angalia kulia. Vuka au geuka kushoto ikiwa ni salama kufanya hivyo.


Lazima madereva wafahamu kwamba magari yanasonga haraka sana katika mazingira haya. Tahadhari na umakinikaji ni muhimu sana. Fahamu kwamba magari marefu, kama vile semis, huenda yasiweze kusimama katika wastani ikiwa wastani ni mwembamba.

## 5.2 KUENDESHA GARI KWENYE BARABARA KUU NA ZA JUU

### VIJIA VYA KUTOKA

Vijia vya kutoka hutumiwa kuingia kwenye barabara za majimbo au barabara kuu na vina sehemu tatu. (Angalia kielelezo cha 5.2)

- 1 **Eneo la kuingilia:** Mpindo huu hukupa muda wa kuchunguza barabara na kutathmini kiasi cha kasi ulicho nacho ili kuingia na kasi inayohitajika.
- 2 **Eneo la kasi na kuungana:** Tumia eneo hili kuendesha gari lako hadi kasi ya magari mengine na ujiunge wakati ni salama kufanya hivyo. Usisimame kabisa kwenye kijia cha kutoka isipokuwa ihtajike kabisa.
- 3 **Sehemu ya kusafiri ya barabara ya majimbo:** Magari ambayo tayari yako kwenye barabara ya majimbo au barabara kuu yanapaswa kusonga, kupunguza kasi au kuongeza kasi ili kuruhusu magari ya kijia cha kutoka kuingia.





Kielelezo cha 5.2: Sehemu za kijia cha kutoka

## 5.3 MIKINGAMO YA KUPUNGUZA MIGONGANO

Mikingamo ya kupunguza migongano imeundwa ili kupunguza idadi ya sehemu za migongano pale ambapo magari yanaweza kugongana. Madereva upande wa barabara wanaotaka kugeuka kushoto au kuvuka barabara kuu ya vijja vinne watageuka kwenye barabara kuu, kujiunga na kijia cha kushoto na kisha wafanye mgeuko wa U katika wastani ulioteuliwa. Mikingamo ya kupunguza migongano huimarisha usalama kwa sababu madereva wanashughulikia tu upande mmoja wa barabara kwenye barabara kuu kwa wakati. Huhitaji kusubiri pengo katika pande zote mbili ili kuvuka barabara kuu. (Angalia kielelezo cha 5.3)

### Kielelezo cha 5.3: Mikingamo ya kupunguza migongano

(Mfano unaonyesha mikingamo ya kupunguza migongano kwenye U.S. 20 na Poplar Ave. katika Kaunti ya Webster) —






## 5.4 KUACHA BARASTE YA ALMASI

Aina hii ya baraste hutumiwa kwenye mkingamo wa baraste mbili za magari ya ukubwa zaidi. Muundo wa kipekee si wa kawaida kwa sababu unaelekeza madereva wa upande mwingine wa barabara kwa muda mfupi kabla ya kuacha njia hadi ndani ya upande sahihi. Kuacha baraste ya almasi hutumia ubora kwa kuhitaji magari kutumia muda mfupi kwenye mkingamo unaodhibitiwa kwa taa ya barabarani. (Angalia kielelezo cha 5.4)

Kielelezo cha 5.4: Kuacha baraste ya almasi  
(Mfano unaonyesha I-35 na First Street ikiacha njia ya baraste ya almasi huko Ankeny.)





## 5.5 MIZUNGUKO

Mizunguko ni mikingamo inayoelekeza magari upande wa mwendo saa karibu na kisiwa cha katikati. Haina alama za kusimama wala taa za barabarani. Alama za kuachia njia, alama za uelekezaji na alama za njia ya miguu huongoza magari kupitia mkingamo. Kwa jumla magari yanaendelea kusonga, lakini kwa kasi ya chini inayopunguza msongamano unaoshuhudiwa katika mikingamo ya kawaida inayodhibitiwa kwa alama za kusimama au taa za barabarani.

### MZUNGUKO WA KIJIA KIMOJA

(angalia kielelezo cha 5.5)

#### Madereva

**Karibia:** Punguza kasi hadi kiwango kilichowekwa na uachie njia wanaotembea katika kivukomilia.

**Ingia:** Unapokaribia alama za mstari wa kuachia njia, achia njia magari yaliyo katika mzunguko. Subiri nafasi iwepo katika barabara, kisha ujiunge kwenye barabara katika mzunguko kwenye mwelekeo wa saa.

**Endelea:** Endelea kwenye mzunguko hadi ufikie barabara yako. Epuka kusimama kwenye mzunguko.

**Toka:** Ashirika kwa taa, kisha toka kwenye mzunguko upande wako wa kulia. Achia njia wanaotembea katika kivukomilia.

#### Wanaotembea

**Karibia:** Kwenye kivukomilia cha wanaotembea, angalia kushoto.

**Vuka:** Vuka hadi kisiwa mgawanyiko kilichonyanyuliwa. Angalia kulia. Kamilisha kuvuka hadi njia ya miguu ya upande mwingine.

#### Waendeshaji baiskeli

Kwa jumla, waendeshaji baiskeli wanapaswa kutembeza baiskeli zao kwenye kivukomilia cha wanaotembea kwa kutumia sheria zilezile kama wanaotembea. Waendeshaji baiskeli wenye ujuzi wanaweza kuvuka mizunguko kama madereva.

Usishike kizuio. Waendeshaji baiskeli wanaotumia mzunguko wanapaswa kufuata sheria zilezile kama madereva. Endesha gari katikati ya kijia ili kuzuia magari kupita. Achia njia wanaotembea katika vivukomilia.

### MZUNGUKO WA VIJIA VINGI


(angalia kielelezo cha 5.6)

#### Mambo ya kufanya


- Unapokaribia mzunguko na kabla ya mstari wa kuachia njia, teua kijia kinachofaa kulingana na alama za kudhibiti vijia na alama za njia ya miguu.
- Unapoingia kwenye mzunguko, achia njia magari yote ambayo tayari yako kwenye mzunguko.
- Baada ya kupita barabara kabla ya njia yako ya kutoka, ashiria kwa taa kwa mgeuko wa kulia, kisha utoke.
- Tahadhari magari katika kijia kingine.

#### Mambo ya kutofanya

- Usibadilisha vijia kwenye mzunguko.
- Usipite wala kuendesha gari kando ya malori au mabasi. Huenda yakamagamaga vijia au yakakosa kukuona.
- Usiendeshe gari nje ya kijia mbali na inavyoruhusiwa. Hii hupunguza ufaafu wa mzunguko na kusababisha hatari kwenye magari yanayotoka kwenye kijia cha ndani kisheria.



Kielelezo cha 5.4: Mzunguko wa kijija kimoja



Kielelezo cha 5.5: Mzunguko wa vijija vingi

## 5.6 KUENDESHA GARI KWENYE BARABARA YA KIJIJINI/CHANGARAWE

Baadhi ya hali za barabara na hatari za kuendesha gari ni za kipekee kwenye changarawe ya kijijini na barabara chafu ikilinganishwa na barabara zilizo na lami. Tahadhari na ufanye mabadiliko kwa ajili ya yafuatayo.

### KUPUNGUA KWA NGUVU

Kuendesha gari kwenye changarawe ni kugumu kuliko kwenye lami kwa sababu magurudumu hayana nguvu zinazohitajika kukupa udhibiti imara. Punguza kasi, epuka kugeuka ghafla, endesha gari na ufunge breki polepole na uongeze umbali wako wa kufuata gari jingine.

### MWONEKANO WENYE VIKWAZO

Miti, mashamba ya mahindi, majengo, vilima na vumbi vinaweza kuzuia mwonekano wa dereva wa magari yanayokuja, au magari yanayoingia kutoka upande. Tambua maeneo yasiyoonekana vizuri ili kutarajia vizuri na kujitayarisha kwa hatari zinazoweza kutokea.

### MIKINGAMO ISIYODHIBITIWA

Mikingamo isiyodhibitiwa ni maarufu zaidi kwenye barabara za changarawe. Haidhibitiwi kwa alama za kuachia njia wala kusimama. Madereva wote wanapaswa kutahadhari, kupunguza kasi na kujitayarisha kusimama kwa ajili ya magari yanayokuja. Kumbuka, huwezi kutegemea mawingu yenye vumbi kuamua ikiwa magari yanayovuka yanakaribia.

**KWENYE MKINGAMO USIYODHIBITIWA, GARI LILIO KUSHOTO LINAPASWA KUACHIA NJIA. USIWAHI KUCHUKULIA KWAMBA MKINGAMO HAUNA MAGARI, AU KWAMBA GARI JINGINE LITASIMAMA.**

### VIJIA VYA DHARURA LAINI

Vijia vya dharura kwenye barabara za vijijini kwa kawaida huwa laini na kutobanana sana kuliko katikati ya barabara. Vijia vya dharura vyenye changarawe/vifusi hufanya magari kuwa magumu zaidi kudhibiti na vitavuta gari lako karibu na mtaro. Punguza kasi wakati wote unapokaribia gari jingine au wakati wowote unapoendesha gari karibu na au kwenye kijija cha dharura cha barabara ya changarawe.

### VUMBI

Tumia taa za mbele za mwangaza wa chini kufanya gari lako lionekane zaidi kwa wengine wakati wa hali za vumbi jingi zaidi.

## KUKUTANA NA MAGARI YANAYOKUJA

Barabara za changarawe za vijijini ni nyembamba na hazina alama za vijia. Punguza kasi na uendelee kwa tahadhari, ukisonga kulia zaidi mradi ni salama kufanya hivyo. Magari mengi husababisha mawingu ya vumbi na kupunguza mwonekano.

## MADARAJA MEMBAMBA

Madereva wanapaswa kutahadhari wakati wanakaribia madaraja membamba. Madaraja mengi kwenye barabara za changarawe za vijijini ni membamba kuliko barabara na yanaweza tu kuwa na gari moja kwa wakati. Jitayarishe kusimama kwa ajili ya magari yanayokuja.

## VILIMA NA MIPINDO MIKALI

Kabla ya kufikia kilele cha kilima au kabla ya kuingia kwenye mpindo, punguza kasi, songa upande wa kulia wa barabara na uangalie magari yanayokuja. Vilima na mipindo kwenye barabara za vijijini mara nyingi ni mikali kuliko kwenye barabara kuu.

## VIVUKO VYA RELI

Punguza kasi wakati wote, angalia pande zote na ujitayarishe kusimama kwa ajili ya gari moshi kabla ya kuvuka reli. Kinyume cha vivuko vingi vya reli kwenye barabara kuu, kwa kawaida hakuna taa nyekundu zinazowaka, kengele za kuonya, malango ya kuvuka wala alama za barabara kwenye vivuko vya reli vijijini.

## MAGARI MAKUBWA NA/AU YANAYOENDA POLEPOLE

Ni kawaida kukutana na magari makubwa na yanayoenda polepole kama vile vifaa vya shambani, ATV/UTV, baiskeli, magari yanayokokotwa na farasi na vifaa vya kukarabati barabara kwenye barabara za vijijini. Ni muhimu kutambua magari haya mapema na kupunguza kasi unapokaribia.

Vifaa vikubwa vya shambani vinaweza kufanya migeuko mipana kwenye njia za kuingia zisizo na alama. Vifaa vingine vya shambani ni vipana kuliko barabara yenyewe. Endelea kwa tahadhari kubwa unapojaribu kupita. Huenda wasione gari lako na vinaweza kuwa vigumu kugundua taa ya kugeuka.



## 5.7 KUENDESHA GARI USIKU

Kumbuka yafuatayo unapoendesha gari kwenye giza.

- Ili kufidia mwonekano uliopungua, punguza kasi yako na uongeze umbali wa kufuata gari jingine.
- Mng'ao mkali wa taa za mbele za magari yanayokuja hufanya kuwa vigumu kuona. Kuangalia upande wa kulia kwa barabara na kurekebisha kioo cha mwonekano wa nyuma kunaweza kusaidia kupunguza mng'ao wa taa za mbele.
- Taa za mbele zinapaswa kuwashwa kabla ya jua kutua ili kulifanya gari lionekane zaidi.
- Mwanga mwingi unapaswa kutumiwa tu wakati madereva wengine hawatauona, kama vile barabara zilizojitenga zenye magari machache.
- Ikiwa taa za mbele za gari jingine zinakufanya kutoona vizuri, punguza kasi na uangalie mstari mweupe kwenye ukingo wa kulia wa barabara ya lami. Taa yenye mwangaza mwingi inaweza kukufanya usione vizuri, lakini hali hiyo hutoweka haraka.





## 5.8 MBAWALA NA WANYAMA WENGINE

Tahadhari wanyama unapoendesha gari, haswa macheo na machweo. **Ukikutana na mnyama na hakuna muda wa kusimama, usiende upande wala kubadilisha welekeo kwa kuwa hatua hii inaweza kusababisha mgongano mbaya zaidi.** Ukimgonga mbawala au mnyama mwingine, fuata itifaki ya mgongano ya kawaida (*angalia sehemu ya 5.15 kwenye ukurasa wa 63*).

Moja ya vyanzo vinavyoongoza vya migongano kwenye barabara za lowa ni wanyamapori, haswa mbawala. Oktoba, Novemba na Mei ni miezi ambayo mbawala wengi hugongwa; hata hivyo, migongano inaweza kutokea wakati wowote wa mwaka. Mbawala hutembea kwenye vikundi, hivyo angalia ikiwa kuna wanyama wengine ukimwona.

## 5.9 KUSHIRIKI BARABARA NA MALORI MAKUBWA

Katika migongano inayohusisha malori makubwa, abiria wa gari dogo haswa dereva, hukumbwa na asilimia 78 na vifo. Ili kujilinda wewe na abiria wengine, tumia tahadhari zaidi unapoendesha gari karibu na malori na mabasi. Kushiriki barabara na magari makubwa kunaweza kuwa hatari ikiwa hufahamu vikomo vyao.

### TAHADHARI MAENEO YASIYOONEKANA VIZURI – “NO-ZONES”

Malori makubwa yana maeneo yasiyoonekana vizuri, au “no-zones,” karibu na sehemu ya mbele, nyuma, na kando ya gari. “No-zones” hizi hufanya kuwa vigumu kwa madereva wa malori kuona. Epuka kujipata katika “no-zone” za malori. Ikiwa huwezi kuona dereva wa lori katika kioo cha lori, dereva wa lori hawezi kukuona. (*Angalia kielelezo cha 5.7*)



Kielelezo cha 5.7: “No-zones” nusu

Mchoro kwa hisani ya FMCSA, [sharetheroadsafely.gov](http://sharetheroadsafely.gov)

### EPUKA HALI ZA KUFUNGA BREKI ZA DHARURA

Malori na mabasi huchukua muda mrefu kusimama ikilinganishwa na magari madogo. Unapopita, angalia mbele ya lori katika kioo chako cha mwonekano wa nyuma kabla ya kuenda mbele na uepuke kusimama mbele ya malori na kusababisha hali ya kufunga breki za ghafla.

### TAHADHARI MALORI YANAYOFANYA MIGEUKO MIPANA YA KULIA

Madereva wa malori wakati mwingine wanahitaji kuenda upande wa kushoto zaidi ili kugeuka kulia vizuri. Hawawezi kuona magari yaliyo nyuma au kando yao moja kwa moja. Kupenya kati ya lori la kichocho kunaongeza uwezekano wa mgongano. Hivyo angalia taa za malori na uyape nafasi ya kutosha ya kugeuka.

## 5.10 KUSHIRIKI BARABARA NA PIKIPIKI

- Heshimu nafasi ya gari ya pikipiki na mkao wake kwenye barabara.
- Mikingamo ni sehemu zinazowezekana zaidi kwa migongano ya gari/pikipiki kutokea. Hakikisha kuwa umeona pikipiki na unajua kasi yake kabla hujaanza kugeuka au kuingia kwenye mkingamo.
- Taa za migeuko hazizimiki kiotomatiki kwenye pikipiki na waendeshaji husahau mara moja moja kuzizima baada ya mgeuko kukamilika. Hakikisha kuwa unajua kile ambacho mwendeshaji atafanya KABLA hujaingia katika njia ya pikipiki.
- Unapoendesha gari nyuma ya pikipiki, acha angalau umbali wa kufuata wa sekunde 3 hadi 4. Hatua hii inampa mwendeshaji nafasi ya kutosha ya kugeuka au kusimama wakati wa dharura. Wakati barabara ina unyevu au ni telezi, kaa mbali zaidi. Pikipiki zinaweza kukosa uthabiti unapojaribu kusimama haraka kwa sababu ni magurudumu mawili pekee yanayokanyaga lami.
- Unapopita pikipiki, ruhusu kijia kamili cha pikipiki; usiwahi kuingia kwenye kijia sawa na pikipiki.
- Tahadhari yasiyotarajiwa na uwape waendeshaji pikipiki sehemu yao ya barabara.

## 5.11 KUSHIRIKI BARABARA NA BAISKELI NA WANAOTEMBEA

### Chunguza barabara uone ikiwa kuna waendeshaji na wanaotembea

Kuwa mwangalifu sana kwa watu wanaotembea na kuendesha baiskeli kabla ya kugeuka kwenye mikingamo na njia za binafsi.

### Achia njia wanaotembea

Angalia taa ya wanaotembea na uachie njia watu wanaotembea.

### Tahadhari wakati unapita magari yaliyosimama

Usiwahi kupita gari jingine ambalo limesimama au linapunguza kasi kwa ajili ya anayetembea. Kumbuka, huenda usiweze kuona anayetembea unapokaribia gari lililosimama, kwa hivyo tahadhari.

### Tahadhari baiskeli

Watu wanaoendesha baiskeli wana haki ya kuwa kwenye barabara na mara nyingi wanapigwa marufuku kuendesha baiskeli kwenye njia za miguu, hivyo heshimu haki yao ya kuwa barabarani.

### Kupita salama

Unapopita waendeshaji baiskeli, lazima ubadilishe vijia kabisa, na kumpa mwendeshaji baiskeli kijia chote kama tu unavyofanya kwa gari jingine lolote. Usigeuke kulia hadi uweze kuona mwendeshaji baiskeli katika kioo chako cha mwonekano wa nyuma.

### Mwonekano

Tahadhari waendeshaji baiskeli usiku na uangalie viakisi au taa zao.

### Angalia maeneo yasiyoonekana vizuri

Tahadhari waendeshaji baiskeli wanaotoka nyuma, haswa kabla ya kugeuka kulia.



## 5.12 MAGARI YALIYOFUNGWA SIKU YENYE JOTO

**USIWAHI kuwaacha watoto, wakongwe, watu wanaotegemea, wala wanyama vipenzi katika gari lililofungwa peke yao.**

Kutegemea na halijoto na unyevu, ndani ya gari mnaweza kuwa na joto juu ya nyuzi 160 chini ya dakika 10. Hata wakati joto ni kidogo, siku yenye nyuzi 78, ndani ya gari lililoegeshwa mnaweza kufika nyuzi 100 kwa dakika chache.

Kuwa kwenye joto kali sana kwa muda mrefu kunaweza kusababisha kiharusi cha joto au kifo. Ukiona mtu aliye na dalili za kiharusi cha joto, pigia simu 911 na uombe huduma za matibabu mara moja. Katika jimbo la Iowa ni halali kwako kuvunja dirisha la gari ili kutoa huduma za matibabu kwa mtu au mnyama aliyekwama ndani.

## 5.13 KUENDESHA GARI KWENYE HALI MBAYA YA HEWA

**Njia bora ya kujitayarisha kuendesha gari kwenye hali mbaya ya hewa ni kuepuka kupatana na mambo usiyotarajia. Fanya utafiti kabla hujaenda ili uweze kuamua ikiwa unahitaji kufanya mabadiliko au kuahirisha safari yako.** Tembelea [511ia.org](http://511ia.org) au pakua programu ya Iowa 511 bila malipo ili kuona taarifa za msafiri kama vile hali za barabara zinazohusiana na hali ya hewa wakati wowote kila siku. 511 pia hutoa picha kutoka kwenye kamera za snowplow zilizowekwa kwenye dashibodi na kamera za barabarani za moja kwa moja ili uweze kuona hali halisi bila kuhitaji kutoka nje. (Angalia kielelezo cha 5.8)

**IKIWA NI LAZIMA UENDESHE GARI KWENYE HALI MBAYA YA HEWA, PUNGUZA KASI NA UONGEZE UMBALI WA KUFUATA GARI JINGINE, HALI INAYOKUPA MUDA ZAIDI WA KUSIMAMA. USITUMIE KIDHIBITI CHA KASI YA GARI WAKATI WA HALI MBAYA YA HEWA.**

Hakikisha kuwa gari lako limejitayarisha kwa hali mbaya yoyote ya hewa kwa kufuata utunzaji wa kawaida (angalia ukurasa wa 22 kwa utunzaji wa gari). Pia ni jambo zuri kubeba vifaa vya hali ya dharura vya gari nyakati zote, haswa majira ya baridi. (Angalia kielelezo cha 5.9)

ANGALIA PICHA ZA KAMERA ZA PLOW ZA WAKATI HALISI KWENYE [511IA.ORG](http://511IA.ORG) AU KATIKA PROGRAMU YA 511



Pakua programu ya Iowa 511

[www.511ia.org](http://www.511ia.org)

Kielelezo cha 5.8: 511 ya hali mbaya ya hewa

Kielelezo cha 5.9: vifaa vya kutumia majira ya baridi



vifaa vya huduma ya kwanz



kimemeshi cha rununu



tangi lililojaa mafuta



maji/vitafunio



kurunzi



buti/glavu/nguo za kuongeza joto



kikwangua barafu/brashi ya theluji



muziki/michezo



kebo za jampa

## BARABA ZENYE UNYEVU/TELEZI

Tahadhari wakati unaendesha gari kabla, wakati wa na baada ya mvua. Mvua inaweza kusababisha kutoweza kuona vizuri, kubadilisha tabia za wengine kuendesha gari na kubadilisha msuguano kati ya gari lako na barabara. Jifunze mambo yafuatayo:

- Washa waipa pindi tu kioo cha mbele cha gari kinapokuwa na unyevu.
- Washa taa za mbele za mwangaza mdogo; hii husaidia wengine kukuona.
- Endesha gari polepole kuliko kawaida na uongeze umbali wako wa kufuata gari jingine hadi sekunde tano au sita.
- Tahadhari sana na upunguze kasi kwenye mipindo na wakati unakaribia mikingamo.
- Washa kiondoa ukungu ili kuzuia madirisha kuwa na ukungu.

### USITUMIE KIDHIBITI CHA KASI KATIKA

### HALI ZENYE UNYEVU/TELEZI.

Ikiwa ni lazima ufanye mabadiliko unapoendesha gari, hakikisha kuwa barabara iliyo mbele haina magari kabla ya kuangalia kwenye dashibodi na uangalie kando kwa sekunde moja au mbili tu.

## KUTELEZA

Kuteleza hutokea kutokana na maji kwenye barabara ambayo ni ya kina zaidi kuliko tredi ya gurudumu. Tabaka hili la maji hupunguza msuguano na magurudumu na linaweza kusababisha kushindwa kudhibiti gari. Ikiwa unaweza kuona maji ya kina kwenye barabara, uakis kwenye barabara, au ikiwa gari lililo mbele haliachi alama kwenye maji, gari lako linaweza kuteleza. Punguza kasi.

## BARABARA ZILIZOFURIKA MAJI

Karibu nusu ya vifo vyote vya mafuriko hutendeka katika magari. Maji yanayosonga yana nguvu nyingi sana na rahisi zaidi kutoyatilia maanani. Maji yaliyo na hadi inchi 6 yanaweza kusomba gari, ikiwa ni pamoja na SUV na pickup.

- Usiwahi kuendesha gari kwenye barabara au daraja lililofurika. Sehemu ya barabara chini ya maji inaweza kusombwa yote. Geuza gari na ufuate njia tofauti.

- Usikae kwenye gari lililofurika maji. Ikiwa gari lako limekwama kwenye maji ya mafuriko, liache na uende sehemu ya juu zaidi.
- Ikiwa gari lako limeingia majini na kuzama, endelea kuwa mtulivu. Subiri gari lijae maji. Pindi gari linapojaa, ni rahisi kufungua milango. Shikilia pumzi na uogelele hadi juu.

## UKUNGU


- Tumia taa za mwanga mdogo au taa za ukungu ikiwa gari lako linazo. Usitumie mwanga mwingi – huakisi ukungu, na kusababisha mng`ao mkali na kutatiza kuona vizuri.
- Punguza kasi hadi kasi yako ilingane na uwezo wako wa kuona.
- Ikihitajika, ondoka barabarani na utafute sehemu salama ya kuegesha gari.

## VIMBUNGA

Huduma ya Hali ya Hewa ya Taifa hutoa “tahadhari” ya kimbunga wakati ngurumo mbaya ya radi inaweza kusababisha hali zinazofanana na kimbunga. Hii inamaanisha kwamba kimbunga kinaweza kutokea. Ikiwa onyo limetolewa, kimbunga kipo karibu na watu wote wanapaswa kutafuta hifadhi mara moja. Matangazo ya runinga, redio za hali ya hewa na ving`ora vya nje vinaweza kufahamisha umma kwamba kuna kimbunga katika eneo hilo.

- Ikiwa unaendesha gari wakati wa kimbunga, hatua bora ni kutafuta hifadhi kwenye jengo thabiti.
- Ikiwa umeshindwa kupata hifadhi, simamisha gari kando, inama chini ya madirisha katika gari, jifunge mkanda na ufunike kichwa chako kwa mikono au kifaa kama vile blanketi au takia.
- Kama njia mbadala, ikiwa unaweza kutoka salama kwenye gari lako, jifiche kwenye mtaro au korongo huku ukifunika kichwa chako kwa mikono au kifaa kingine.
- Kaa mbali na madaraja na tambukabaraste.

**Kielelezo cha 5.10: Barafu inajitengeneza kwenye madaraja kwanza kutokana na hewa inayozunguka juu na chini ya barabara.**



## BARAFU NA THELUJI

- Hakikisha kuwa gari lako LOTE halina theluji na barafu kabla ya kuliendesha, hii ni pamoja na madirisha, taa za mbele, taa za migeuko na taa za nyuma.
- Tahadhari barafu nyeusi. Wakati halijoto inapungua, unyevu unaweza kubadilika na kuwa barafu kwenye barabara. Mara nyingi barafu hii inaitwa barafu nyeusi kwa sababu ni nadra kuonekana na mara nyingi huwashangaza madereva. Barafu nyeusi inaweza kutokea mahali popote, lakini huwa maarufu kwenye madaraja na tambukabaraste, ambapo unyevu huganda haraka kutokana na hewa inayozunguka juu na chini ya barabara. Kutokana na hali hii, madaraja na tambukabaraste zinaweza kuwa telezi hata wakati sehemu nyingine za juu za barabara si telezi. (*Angalia kielelezo cha 5.10*)
- Unapoanza kuendesha gari kutoka mkao wa kusimama, nyosha magurudumu na uendeshe taratibu ili kuepuka kuzungusha magurudumu.
- Punguza kasi yako ili kufidia upotezaji wa nguvu.
- Usitumie kidhibiti cha kasi katika hali zenye barafu au theluji.
- Anza kupunguza kasi kabla ya kutarajia kusimama kwenye mkingamo au mgeuko. Funga breki tu wakati unasafiri kwenye mstari wima. Umbali wa kusimama unaweza kuwa mkubwa mara 10 katika barafu na theluji.
- Kaa nyuma kabisa ya gari lililo mbele ili usilazimike kusimama ghafla, hali inayoweza kusababisha kuteleza.

## Kushiriki barabara na snowplow

Ikiwa unaendesha gari majira ya baridi kaitika jimbo la Iowa, uwezekano ni kwamba utakuwa ukishiriki barabara na snowplow wakati fulani.

- **Tahadhari unapokaribia snowplow.** Snowplow kwa kawaida hufanya kazi kwa maili 25 hadi 35 kwa saa. Madereva wengi hushindwa kutambua hili na kuzigonga kwa nyuma.
- **Usiwahi kupita upande wa kijia cha dharura wa plow.** Plow zitasogeza theluji kwenye vijia vya dharura.
- **Zipe nafasi zifanye kazi.** Snowplow zina maeneo makubwa yasiyoonekana vizuri na zinaweza kuchukua wingu la theluji lililo karibu nazo na kukutatiza kuona na hizo kukuona. Ni vizuri kukaa nyuma na kuvumilia hadi uweze kupita salama.
- **Acha nafasi ya kutosha unapopita.** Mabapa ya plow yanaweza kuwa yamechomoka zaidi ya upana wa gari la plow.

## Kukwama katika theluji

Hivi hapa vidokezo endapo utakwama katika theluji.

- Ikiwezekana, weka gari lako kwenye kijia cha dharura na usalie ndani ili kuepuka kugongwa na magari mengine.
- Pigia simu 911 kwa usaidizi wa dharura. Ili kusaidia kuelekeza wahudumu wa dharura hadi mahali ulipo, tafuta nambari za kutoka, machapisho ya maili, njia panda, au minara.
- **Eneo salama zaidi ni kusalia ndani ya gari lako ukiwa umejifunga mkanda.** Gari lako ni hifadhi unayoweza kuhitaji ili kuponea na hukuruhusu kupatikana na watumishi wa uokoaji.

## 5.14 DHARURA ZA VIFAA KUACHA KUFANYA KAZI

Haijalishi jinsi ulivyo mwangalifu, wakati fulani huenda ukajipata katika hali ya dharura. Ikiwa umejitayarisha, unaweza kuzuia matokeo yoyote mabaya.



### GURUDUMU KUISHA PUMZI

Gurudumu lako likiisha pumzi ghafla:

- Shikilia usukani kwa nguvu na uendeshe gari mfululizo.
- Punguza kasi taratibu. Ondoa mguu kwenye pedali ya mafuta na ufunge breki kidogo.
- Usisimame barabarani ikiwezekana. Ondoka barabarani hadi sehemu salama.

Gurudumu la mbele likitoa pumzi, dharura inaweza kuwa kubwa zaidi. Kutoa pumzi kwa gurudumu la mbele kutashtua gari vibaya zaidi kuelekea upande wa gari ulioisha pumzi. Kuwa mwangalifu kutorekebisha zaidi wakati unaendesha baada ya gurudumu la mbele kutoa pumzi. Jaribu kunyosha gari, kisha usonge taratibu kwenye kijia cha dharura cha kulia cha barabara haraka iwezekanavyo.

### TAA

Taa zako za mbele zikiacha kuwaka ghafla:

- Jaribu swichi ya taa za mbele mara kadhaa.
- Jaribu kuwasha taa zako za mwanga mwingi.
- Washa vimweko vya dharura, taa za migeuko, au taa za ukungu ikiwa taa za mbele haziwaki tena unapojaribu swichi ya taa za mbele.
- Ondoa gari barabarani haraka iwezekanavyo.

### MTAMBO KUKWAMA

Mtambo ukikwama unapoendesha gari:

- Shika usukani kwa nguvu. Usukani utakuwa mgumu kugeuka, lakini unaweza kuugeza.
- Ondoa gari barabarani. Breki bado zitafanya kazi, lakini utahitaji kusukuma kwa nguvu sana kwenye pedali ya breki.

### PEDALI YA MAFUTA KUKWAMA

Ikiwa gari halipunguzi kasi, au linaongeza kasi unapoondoa mguu kwenye kichapuzi:

- Tupa macho barabarani.
- Badilisha haraka hadi neutral.
- Ondoa gari barabarani wakati ni salama kufanya hivyo.
- Zima mtambo bada ya kusimama.

### MIFUMO YA KUFULI LA USUKANI

Magari mengi yamewekwa mifumo ya kufuli la usukani inayokusudiwa kuzuia wizi. Usiwahi kuondoa ufunguo wala kuruhusu abiria kugusa ufunguo unapoendesha gari. Ufunguo ukiondolewa, usukani utajifunga. Hatua hii inaweza kusababisha kushindwa kudhibiti gari na mgongano.

### BREKI KUACHA KUFANYA KAZI

Breki zako zikiacha kufanya kazi:

- Sukuma pedali ya breki mara kadhaa. Hatua hii mara nyingi hujenga kani ya breki ya kutosha ili kukuruhusu kusimama.
- Ikiwa hatua hiyo haitafanya kazi, tumia breki ya kuegesha. Vuta breki ya kuegesha taratibu ili usifunge magurudumu ya nyuma na kusababisha utelezaji. Kuwa tayari kuachilia breki gari likianza kuteleza.
- Ikiwa hatua hiyo haitafanya kazi, anza kubadilisha hadi gia za nyuma na utafute sehemu nzuri ili upunguze kasi usimamisha gari. Hakikisha kuwa umeondoa gari lako barabarani. Usiendeshe gari bila breki.

## 5.15 KUHUSIKA KATIKA AJALI

Kuhusika katika ajali linaweza kuwa jambo la kutia wasiwasi, hata iwe ndogo zaidi. Lengo kuu la kutathmini ajali yoyote ni kuhakikisha kuwa madereva na abiria wote wako salama. Tumia yafuatayo kama mwongozo wa jambo la kufanya wakati wa ajali.



### HATUA YA 1: ONDOA GARI BARABARANI UNAPOPATA AJALI

Ikiwezekana, hakikisha kuwa gari lako limetoka barabarani, limezimwa na halisongi tena.



### HATUA YA 2: WASILIANA NA MAMLAKA YA UTEKELEZAJI SHERIA

Wasiliana na mamlaka ya utekelezaji sheria ili kuripoti ajali kwa kupigia simu 911. Hakikisha kuwa umetoa maelezo mengi zaidi iwezekanavyo ikiwa ni pamoja na majeraha na eneo la ajali.

Ni sheria ya jimbo kuripoti ajali kwa polisi inayohusisha majeraha au kifo kwa mtu mwingine, au uharibifu wa mali wa zaidi ya dola 1,500. Kukosa kufanya hivyo ndani ya saa 72 za tukio kutasababisha kupoteza haki zako za kuendesha gari na adhabu zaidi.



### HATUA YA 3: YAPE MAMLAKA YA UTEKELEZAJI SHERIA MAELEZO YA BIMA NA MAWASILIANO

Kuwa tayari kumpa afisa wa utekelezaji sheria:

- Maelezo ya bima ya gari
- Usajili wa gari
- Leseni ya dereva




### HATUA YA 4: RIPOTI KWENYE KAMPUNI YA BIMA

Rejelea bima yako ya dhima kutathmini gharama ambazo zitahitaji kulipwa na kile ambacho unastahiki kupata. Endapo utasemekana una makosa katika ajali inayohusisha dereva mwingine, utahitaji kujadili gharama ambazo utahitajika kumfidia pia.

## 5.16 MAZUNGUMZO NA MAMLAKA YA UTEKELEZAJI SHERIA

Unaweza kuzungumza na mamlaka ya utekelezaji sheria kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamishwa barabarani. Unapozungumza na afisa wa utekelezaji sheria, kuwa mtulivu na ufuate maagizo.

Ikiwa una ugonjwa wa akili na/au wewe ni kiziwi au una matatizo ya kusikia, unaweza kuweka kiashiria kwenye leseni au kitambulisho chako. Aina hii ya kiashiria huchapishwa kwenye leseni/kitambulisho chako na pia kitaonekana katika hifadhidata inayotumiwa na mamlaka ya utekelezaji sheria ili kutafuta maelezo ya dereva wakati wa kusimamishwa barabarani. Hatua hii husaidia afisa kujitayarisha vizuri kuzungumza nawe.



Kielelezo cha 5.11: Kiashiria cha spektra za ugonjwa wa akili na kiashiria cha kiziwi au matatizo ya kusikia

### KUSIMAMISHWA BARABARANI

Ukiona gari rasmi la mamlaka ya utekelezaji sheria likikuashiria usimame, ondoa gari barabarani kwa uangalifu hadi eneo lisilo na magari ikiwa salama. Usimame kwenye kijia cha magari. Kwenye barabara zenye magari mengi au barabara kuu, inaweza kuwa salama zaidi kugesha kwenye maegesho au kwenye barabara isiyo na magari mengi. Zima gari lako, weka mikono yako mahali inapoonekana (inapendekezwa kwenye usukani), kuwa mtulivu, na ufuate maagizo ya afisa.

Afisa anaweza kumwomba dereva au abiria wajitambulisha (jina, tarehe ya kuzaliwa, n.k.) na kutoa leseni au kitambulisho, thibitisho la bima, na usajili wa gari. Weka hati hizi karibu katika sehemu moja ndani ya gari na usubiri afisa aombe hati hizo kabla hujazileta.

Endapo utapokea tikiti ya barabarani, kubali tikiti hiyo bila tatizo. Kutia sahihi tikiti ya barabarani hakumaanishi kuwa unakubali kosa, kunathibitisha tu kuwa umeipokea.



*Ukurasa huu umeachwa mtupu makusudi.*





# UKO TAYARI KWA MTIHANI WAKO?

Fanya mtihani wetu wa maarifa mtandaoni kwenye  
[iowadot.gov/mvd/driverslicense/manuals-and-practice-tests](https://iowadot.gov/mvd/driverslicense/manuals-and-practice-tests)  
kisha uweke miadi ya kufanya mtihani rasmi.

Tunasubiri kwa hamu kukuona barabarani ukiendesha gari salama.

---

## JE, UNAHITAJI MWONGOZO HUU KATIKA LUGHA TOFAUTI?

Mwongozo huu umetafsiriwa katika lugha za ziada zinazopatikana kwenye:  
[iowadot.gov/mvd/driverslicense/driverslicense/dlmanual](https://iowadot.gov/mvd/driverslicense/driverslicense/dlmanual)





---

Maelezo yaliyo katika mwongozo huu ni kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Usimamizi za Iowa.

[www.legis.iowa.gov/law/iowaCode](http://www.legis.iowa.gov/law/iowaCode)

[www.legis.iowa.gov/law/administrativeRules](http://www.legis.iowa.gov/law/administrativeRules)

---

Iowa DOT huhakikisha kutokuwepo kwa ubaguzi na ajira kwa wote katika mipango na shughuli kwa mujibu wa Title VI na Title VII za Sheria ya Haki za Raia ya 1964 na sheria nyingine zisizo za ubaguzi. Ikiwa unahitaji maelezo zaidi au usaidizi maalum kwa watu walio na ulemavu au wanaofahamu Kiingereza kidogo, wasiliana na Iowa DOT Civil Rights kwa nambari 515-239-1111 au kwa barua pepe kwenye [civil.rights@iowadot.us](mailto:civil.rights@iowadot.us).



---

IOWA DEPARTMENT OF TRANSPORTATION